Nipashe
Jumanne Novemba 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580409
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**SHIRECU** yarejeshewa mali ilizoporwa nchini
UKURASA 2



**UHAMASISHAJI** madawati kijinsia vyuoni waanza
UKURASA 3



UKURASA 11

# Hiace ilivyoua watu wanane

• **Sita** wajeruhiwa, ni baada ya kutumbukia shimoni, mashuhuda wasimulia... *Endelea ukurasa 3*



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akipiga picha ya 'selfie', baada ya kufungua mkutano wa jukwaa la vijana wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ulioandaliwa na Kituo cha Kimataifa cha Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii, Utawala Bora na Uongozi na jumuiya hiyo, jijini Arusha jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

RIPOTI MAALUMU

## Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo watoto -2

UKURASA 4

## Wanaolangua saruji watangaziwa kiama

UKURASA 2


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**MICHEZO** **FIFA YAMFUNGIA RAIS CAF MIAKA 5** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, alipofika Ikulu, Zanzibar mwishoni mwa wiki kwa mazungumzo. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko, Juanita Mramba. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wanaolangua saruji watangaziwa kiama

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

WAFANYABIASHARA wanaouza saruji kwa bei ya ulanguzi, wameonywa kuchukuliwa hatua kadhaa, ikiwamo kushtakiwa na kufungiwa biashara.

Onyo hilo limetolewa na serikali mkoani Morogoro, kutokana na bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei ya juu.

Serikali imesema itawachukulia hatua wafanyabiashara wote wa saruji, ambao wanauza bidhaa hiyo kwa bei ya Sh. 25,000 ikiwamo kuwafikisha mahakamani kwa kesi ya uhujumu uchumi.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mkoa huo, kuhusiana na kupanda kwa bei ya saruji bila sababu za msingi.

Alisema serikali imefanya uchunguzi na kubaini kuwa Manispaa ya Morogoro ndio inaongoza kwa kuuza saruji bei ya juu kulinganisha na maeneo mengine, jambo ambalo haliwezi kukubalika.

"Manispaa ya Morogoro ndio ya kwanza kupandisha bei, inauzwa kwa bei ya Sh. 25,000...hao wachache wanataka kutuharibia mambo hapa tumeshafanya utafiti na tumewabaini," alisema Sanare.

Alisema kuwa utaratibu wa kuwachukulia hatua wafanyabiashara hao, utaanza muda mfupi baada ya uchunguzi kukamilika, na licha ya kuwafikisha mahakamani pia biashara zao zitafungwa.

Aliongeza kuwa ameshatoa maelekezo kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) mkoani humo, kwamba atakayekamatwa kwa kosa hilo afutiwe leseni ya kufanya biashara ya saruji.

Kwa upande wao baadhi ya wafanyabiashara mkoani Morogoro walioomba serikali kuzuia kusafirishwa saruji nje ya nchi, ili ipatikane kirahisi zikiwa jitihada za kukabiliana na mfumuko wa bei.

Thabit Islam, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema kuwa miongoni mwa sababu zinazosababisha kuongezeka kwa gharama ni uwapo wa foleni kubwa viwandani katika upakiaji wa mizigo na kusababisha magari kutumia muda mrefu safarini.

"Tunaomba serikali izuie kuuza nje ili hapa kwetu ipatikane kirahisi, unakuta gari inakaa zaidi ya siku 14 kwenye kiwanda kutokana na magari ya nje ya nchi kuja kwa wingi, kwa sababu kwenye nchi zao huko viwanda vyao vimefungwa kwa sababu bado wanasumbuliwa na magonjwa," alisema Islam.

# SHIRECU yakabidhiwa mali ilizoporwa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

CHAMA Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (SHIRECU), kimekabidhiwa hati saba za mali za viwanja na nyumba, zilizoporwa na kuuzwa kinyume cha utaratibu.

Mwenyekiti wa timu iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, kufuatilia mali zilizoporwa za SHIRECU, Asangy Bangu, alisema jana kuwa wamefanikiwa kurudisha viwanja saba, pamoja na nyumba ambazo ni mali za SHIRECU.

Alisema wamefanikiwa kurudisha viwanja saba vilivyopo mkoani Shinyanga, nyumba ya ghorofa tatu ambayo ipo Ilala, pamoja na ghala lililopo Kurasini jijini Dar es Salaam, ambazo ni mali za SHIRECU.

"Leo tunakabidhi hati saba za mali za SHIRECU, ambazo ziliuzwa kinyume cha taratibu, kuwa rasmi mali za chama hiki, na zoezi hili litakuwa endelevu ili kurudisha mali zote," alisema Bangu.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, aliipongeza timu hiyo kwa kufanya kazi kwa uzalendo, ambayo ilikuwa na mizengwe mingi, huku akiutaka uongozi wa SHIRECU, kuzitunza mali hizo na zisiweze kurudi tena mikononi mwa watu binafsi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alitaka watu ambao waliuza mali hizo za SHIRECU na kuisababishia hasara kubwa wawajibishwe, ili kuwa mfano kwa watumishi wengine.

Pia, alikitaka chama hicho baada ya kupata mali hizo, kijiendeshe kibiashara pamoja na kukuza miradi yao kuinuka kiuchumi, ikiwamo Shule ya Sekondari Buluba, kurudi kwenye hadhi yake ya kufaulisha kwa kuajiri walimu wenye sifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa SHIRECU, mkoani Shinyanga, Lenis Jishanga, aliishukuru timu hiyo kuwarudishia mali zao, na kuahidi kuzitunza pamoja na kujiendesha kibiashara zaidi.

# JK ataka vijana kushiriki mchakato mtangamano EAC

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, amelitaka kundi la vijana wa nchi wanachama wa Jumuiya Afrika ya Mashariki (EAC) kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa mtangamano wa jumuiya hiyo kutokana na wingi wao.

Kikwete aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Makao Makuu wa EAC jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa siku tano wa jukwaa la vijana la EAC linalofahamika Kama "YouLead" ulioandaliwa na Kituo cha Maendeleo, Uongozi na Utawala Bora cha MS TC DC na EAC.

Alisema vijana ni kundi kubwa linalofikia asilimia 80 ya watu wote wa jumuiya, hivyo ni vyema wakashiriki kwa nguvu zote ili mawazo mengi yenye tija yaweze kuongeza chachu, lakini uimara wa mchakato wa kuifikisha EAC kwenye mtangamano kamili.

"Wasome mkataba una kila kitu, wajue kinachoendelea na kinachokusudiwa, sauti ya vijana ni muhimu katika ujenzi wa jumuiya," alieleza.

Mkurugenzi wa Programu wa MS TC DC, Sara Teri, alisema siku tano za mkutano watajadili ajenda za vijana kichumi kisiasa, kijamii na usalama, biashara zitakapomazilika Ijumaa wiki hii, vijana watakuwa na mkusanyiko na kuhitimisha maazimio kuhusiana na masuala waliyojadili.

Naye Mwenyekiti wa Bunge la zamani la Vijana la EAC, Abdilahi Lugome, aliwataka vijana wa Tanzania kuchangamkia fursa zilizopo pamoja na kupigania kuanzishwa kwa Jukwa la Vijana Tanzania.

Alimwomba Rais John Magufuli kusaidia kuanzishwa kwa baraza kwani sheria ambayo ilishatungwa imetamka juu ya kuanzishwa kwa jukwaa hilo, ingawa utekelezaji bado.

## HABARI KITAIFA




Msemaji wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee, Prudence Constantine (wa pili kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, utakaofanyika kesho, jijini humo. Wengine ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Msaada wa Sheria ya LSF, Lulu Ngwanakilala (kushoto), Dk. Wilfred Ochan kutoka UNFPA (kulia) na Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanane wafariki dunia kwenye ajali

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

WATU wanane wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa baada ya gari yenye namba za usajili T.471 DGC, Toyota Hiace inayofanya safari zake kati ya Kemondo wilayani Bukoba kwenda Bukoba mjini mkoani Kagera, kupoteza mwelekeo na kutumbukia kwenye shimo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva kushindwa kufunga breki na kuparamia watembea kwa miguu.

Wakizungumza na Nipashe eneo la tukio, baadhi ya mashuhuda walisema baada ya gari hiyo kupoteza mwelekeo liliwagonga watu hao.

Shuhuda Riclain Ndostaini, alisema alikuwa barabarani kuelekea nyumbani na kushuhudia mama mmoja akivuka barabara kupisha gari hilo, lililokuwa likiendeshwa kwa kasi ambalo lilimgonga na kufariki dunia papo hapo.

"Mama huyo alikuwa akitokea maeneo ya sokoni wakati anavuka barabara nikaona anagongwa na gari hilo. Mwili ulikuwa unaburuzwa na ndani ya gari walikuwa watu wanne ambao tumewaokoa mmoja alikuwa amesha kufa, mwingine ameumia mkono mmoja ameangukia shimoni," alisema Ndostaini.

Mganga aliyepokea majeruhi wa ajali hiyo, Dk. Yustas Tibanga, alisema walipokea marehemu sita na majeruhi wanane.

Kamanda Malimi, alisema, tukio hilo lilitokea Novemba 22, saa 2:00 usiku eneo la Kata ya Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba.

"Dereva Ismail Rashid (37), mkazi wa Kemondo ni majeruhi lakini atakuwa chini ya ulinzi ili taratibu nyingine ziweze kufuatwa baada ya kupatiwa matibabu kwani alikuwa mwendo kasi na kusababisha ajali kubwa kama hii ambayo ni ya pili kutokea kwa matukio ya ajali ya kupoteza watu," alisema Malimi.

Malimi alisema, baada ya dereva huyo kuona hitilafu imetokea na kushindwa kulimudu gari, alilishusha kwenye mteremko mkali ng'ambo ya barabara ambako kuna shimo na kutumbukia.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Charels Kahigi, alisema vifo vingine vimeongezeka kutoka watu sita hadi wanane na majeruhi sita.

Alitaja majina ya marehemu waliotambuliwa kuwa ni Rausati Khalfan (35), Rehema Abubakari (30), Jonson John (26), Anchila Rweyendele (62) na Retisia Grayson (58), Dominick Kibuka (48),

Taarifa iliyotolewa na Kamanda Malimi, ilisema majeruhi waliobaki hospitali ni sita kati ya hao, watano wametambulika na mmoja wa kiume hajatambulika, ambaye hali yake ni mahututi.

Aliwataja waliotambuliwa kuwa ni Ashirafu Maulid (28), Bahati Mapipi (23), Rods John Bosco (20), Vedasto Liberatus (25) na Johannes Gilbert (20).

# Uhamasishaji madawati ya kijinsia vyuoni waanza

**Na Romana Mallya**

SIKU 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa mwaka huu zinaadhimishwa kwa kuhamasisha uanzishwaji wa madawati ya kijinsia vyuoni.

Madawati hayo yatasaidia wanafunzi wanapokutana na ukatili kupeleka malalamiko yao na hatua kuchukuliwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WILDAF), Anna Kulaya, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mafunzo ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyoandaliwa na shirika hilo na wadau wengine na kutolewa kwa wahariri na waandishi wa habari.

Kulaya alisema maadhimisho ya mwaka huu watayatumia kupita mikoa mbalimbali wadau ikiwamo vyuoni kutoa elimu kuhusu kuanzishwa kwa madawati hayo.

Alisema takwimu zinaonyesha kati ya matukio 11,726 yaliyoripotiwa, matukio ya ubakaji ni 7,617 sawa na asilimia 64.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Kulaya alisema maadhimisho ya mwaka huu yatafanyika kwa kuwa na matukio tofauti ikiwamo misafara itakayopita maeneo mbalimbali mikoani na kwenda vyuoni ili kuhakikisha kunaanzishwa madawati maalum ambayo yatawezesha wanaofanyiwa vitendo hivyo kupeleka malalamiko yao.

"Ripoti ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeonyesha asilimia 50 ya waliohojiwa wameeleza rushwa ya ngono vyuoni.

"Ndiyo maana katika maadhimisho ya mwaka huu yaliyobebwa na kauli mbinu isemayo, 'Tupinge ukatili wa kijinsia mabadiliko yanaanza na mimi' tumeona pamoja na mambo mengine tuende vyuoni kuzungumza nao pindi wanapokutana na vitendo hivyo wachukue hatua ya kutoa taarifa."

Alisema baada ya mafunzo hayo yaliyotolewa kwa wahariri na waandishi wa habari, Jumatano itakuwa ni Siku ya Kimataifa ya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

Aliongeza kuwa ndani ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kutakuwa na tuzo kwa wanawake 16 waliotoa maisha yao kutetea wanawake wengine.

Kadhalika, alisema wataangalia ukatili wa kijinsia unaotokea nyumbani kwa sababu ni moja ya maeneo ambayo yanatakiwa kuwa salama.

Vilevile, alihimiza jamii kuhakikisha inapaza sauti na kufanya mabadiliko maeneo yao.

Mkuu wa Mawasiliano serikalini kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Prudence Constantine, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa sasa vimevuka mipaka na sasa kuna ukatili wa kisaikolojia unaowahusisha jinsia zote, lakini taarifa zake siyo za kutosha.

"Serikali imechukua hatua mbalimbali ya kutokomeza vitendo hivi. Upo mpango wa kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, tunampango wa kupunguza ukatili kwa asilimia 50.

"Yapo madawati ya kijinsia 450 yaliyoanzishwa vituo vya Polisi kwa ajili ya kupokea taarifa za ukatili wa kijinsia, waathirika 58,059 wamejitokeza kutoa taarifa."

Pia alisema magereza nao wameanzisha madawati 162 nchini.

Ofisa Mtendaji wa Taasisi ya Msaada wa Kisheria (LSF), Lulu Ng'wanakilala, alisema mikakati ni kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia nchini na siyo kupunguza.

# Jela miaka 5 kwa wizi wa magodoro shuleni

**Na Samson Chacha, TARIME**

MKAZI wa Mtaa wa Serengeti Mjini Tarime mkoani Mara, Francis Chacha Mokera (18), amehukumiwa kwenda jela miaka mitano baada ya kupatikana na hatia ya kuvunja na kuiba mali za Shule ya Sekondari Tarime zenye thamani ya Sh. 2,850,000.

Mahakama ilimkuta Chacha na hatia ya kuiba mali hizo ambazo ni magodoro, viti na taa za umeme.

Akisomewa hukumu hiyo katika kesi ya jinai namba 155/2020 Novemba 20, 2020, Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Vicensia Balyahula, alisema kuwa ameridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila kuacha shaka yoyote.

Awali mwendesha mashtaka wa Polisi, Thabiti Temba, alidai kuwa mshtakiwa alitenda wizi huo kwa kuvunja milango ya Shule ya Sekondari Tarime na kuiba magodoro, viti vya chuma na taa za umeme, vyote vikiwa na thamani ya kiasi hicho cha fedha kwa nyakati tofauti katika kipindi cha Machi na Mei 2020 na kusababisha hasara kwa shule hiyo pamoja na wanafunzi kuathirika kimasomo.

Hakimu Vicensia alisema vitendo hivyo vya wizi, katika shule ni hujuma, hivyo nakuhukumu kwenda kutumikia kifungo cha miaka mitano jela ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaohujumu mali za umma.


**UBALOZI WA MAREKANI DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

UNIVERSAL AUCTION CENTRE Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani/Ofisi na Magari tarehe 28 November, 2020 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fenicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Chest drawer, Wardrobe, Dressers, China base, Hutch, Credenza, Dining Table, Chair,Office Desk, Chair, Book case, Garden Table, Chair, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge, Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya umeme, A/c split units, Photocopy Machine na vingine vingi

.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6.00 mchana.**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Hilux Double Cabin 4X4 | 2KD Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 2 | Nissan Min Bus | ZD30 Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 3 | Suzuki Jimmy Station Wagon 4x4 | M13A Petrol Engine | 2014 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza, Lion Street kuanzia tarehe 26 mpaka 27 November 2020 ,saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa mweka hazina (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 3 December, 2020 saa 10:00 jioni, ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB bank na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926, 0757 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com DAR ES SALAAM**



Baadhi ya watoto wa kituo cha kulelea yatima cha Bunju A, wakiwa katika shughuli mbalimbali wanazofundishwa kituoni hapo. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

# Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo vya watoto - 2

**Na Elizabeth Zaya**

***KATIKA sehemu ya kwanza tuliona athari za corona katika vituo vya kulea watoto yatima, hali ilivyo na jinsi maisha yalivyogeuka kuwa shubiri huku wafadhili wakikata misaada. Endelea sehemu ya II ya ripoti hii.***

MKURUGENZI Mtendaji wa kituo cha kulelea watoto cha Mwandaliwa, Haji Bakhulla, anasema mmiliki wa kituo hicho alishafariki na yeye amekuwa baba wa watoto hao kwa kuziba pengo.

"Nimebaki kama mlezi mkuu wa kituo, nilipoona hali imezidi kuwa mbaya ilinibidi nitumie hata bajeti ya familia yangu nyumbani kwa ajili ya kuhudumia kituo ili kuhakikisha kwamba watoto wanapata chakula, na tunavyozungumza hivi nilimaliza akiba yote ya familia."

"Nilifanya hivyo kwa sababu tayari nao ni familia yangu na ndiyo maana kunapokosekana chakula kwenye kituo napata mawazo zaidi na tayari nimeshajizatiti kufanya kazi ya Mwenyezi Mungu ya kuwasaidia watoto hawa ambao hawana hatia."

**MLO WABADILIKA**

Walikuwa wakijipangia ratiba ya chakula cha watoto wanavyotaka ili kuwafurahisha na kuwafanya wajione kama wengine wanaoishi na wazazi wao.

Ratiba ilikuwa Ijumaa, Jumatano na Jumapili, chakula kikuu ni wali na nyama pamoja na mboga za majani, lakini baada ya msukosuko ratiba ilibadilika.

Baada ya kupata athari walianza kupika ugali, maharagwe na dagaa kila siku isipokuwa mara moja moja wanapobahatika kupata mchele walikuwa wanawapikia wali na maharagwe kwa Jumapili pekee.

Bakhulla anaeleza kwamba kutokana na hali kuwa mbaya walilazimika kuwaita watoto wakubwa kidogo ili kuwaeleza hali halisi ya hali ngumu wanayopitia katika kituo na kwamba wanashukuru walielewa.

"Wale wakubwa kidogo wenye uelewa walielewa tulipowaambia, lakini shida ilikuwa ni kwa wale wadogo kabisa. Wengine walikuwa wanalia hasa inapobidi kuwapikia chakula ambacho hawajakizoea, ilibidi tuwalazimishe ili wasilale na njaa."

**WAGEUKIA KILIMO**

Katibu wa Kituo hicho cha Mwandaliwa, Omari Kyaruzi, anasema kituo hicho kina shamba kwa hiyo waliamua kuanza kulima mboga za majani ili ziwasaidie kukidhi mahitaji ya chakula.

**WAFANYAKAZI WAKIMBIA**

Kyaruzi anasema kutokana na msukosuko huo, walishindwa kuwalipa wafanyakazi waliokuwa wanasaidia kazi za kuwalea watoto kituoni hapo.

"Tulikuwa na wafanyakazi 12, kwa hiyo baada ya hali kuwa ngumu, watano walikimbia tukabaki nao saba kwa sababu tulishindwa kuwalipa mishahara yao, japokuwa tuliwaeleza kwamba hali ikitengamaa tutawalipa, lakini walisema na wao wana familia na wanatakiwa waziendeshe kwa hiyo waliamua kuacha," anasema Kyaruzi.

"Ilibidi nimwombea mke wangu atusaidie kwa kipindi chote chenye shida na akakubali, kadhalika na Mkurugenzi naye ilibidi amwombe mke wake waendelee kutusaidia pale wanapokuwa na muda mpaka sasa."

WASHINDWA KUWAPELEKA SHULE

Katika kipindi hicho cha mlipuko wa corona, walipelekewa watoto wengine wanne ambao baada ya serikali kufungua shule wangetakiwa wawapeleke shule za ufundi, lakini walishindwa kufanya hivyo kwa sababu ya kukosekana ada ya kuwalipia.

"Kama kawaida kwa sababu kituo chetu kinafahamika, tuliletewa watoto wengine katikati ya kipindi cha corona, ni wadogo wana miaka 13 na 15 walifanyiwa vitendo vya ukatili na walikuwa hawasomi.

"Tulipanga kwamba endapo mambo yakienda vizuri tuwapeleke wakasome ufundi kuliko kukaa bure wasijue chochote, lakini tumeshindwa kwa kukosa fedha ya kuwalipia ada, lakini tukijaliwa tutawapeleka," anafafanua.

**MATIBABU**

Kyaruzi anasema wana ahueni ya msaada hospitali kubwa binafsi iliyopo Namanga Kinondoni, Dar es Salaam, iliyojitolea kuhudumia yatima hao.

Licha ya msaada huo, hali bado tete na kwamba wahisani wa nje waliokuwa wanawategemea kwa misaada, kwa kiwango kikubwa hawajaanza kuwasaidia.

"Bado tunaendelea kuwalea watoto wetu kwa utaratibu ule ule wa kupiga simu kwa wadau wetu kuwaomba msaada na wakati mwingine kwenda katika ofisi mbalimbali kuwaomba," anasema Kyaruzi.

**KUNA AHUENI?**

"Wafadhili mmoja mmoja sana hasa hizi taasisi za dini ndio angalau wanakuja," anasema na kuongeza:

"Au ukienda kuwaomba wanajitahidi kutusaidia japokuwa siyo kila siku, hakuna kitu kilichobadilika kuondoa athari ambazo tumezipata!"

"Tunaamini kwamba mambo yatakaa sawa muda si mrefu kwa sababu nchi nyingi zimefungulia mipaka yake. Tunapongeza juhudi ambazo zimechukuliwa na serikali yetu kwa sababu bila hivyo hali ingekuwa ngumu zaidi ya hapa."

**MMILIKI APOTEZA UJAUZITO**

Mmoja wa wamiliki wa kituo cha kulelea watoto cha Ikwiriri eneo la Kazamoyo, mkoani Pwani ambaye hakupenda kitajwe wala majina yake kutajwa gazetini, anasema kwamba na yeye alikuwa anategemea msaada kutoka kwa wahisani wa mataifa ya nje kwa asilimia kubwa kuwalea watoto hao.

Anasema baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa corona duniani na wahisani kusitisha safari za kuja nchini na misaada tangu Desemba, mwaka jana alilazimika kutumia rasilimali zake ikiwamo kuuza eneo lake la ardhi kwa ajili ya kupata pesa ya kusaidia kuhudumia watoto hao.

"Lakini pamoja na kufanya hayo yote pesa yote ilikwisha na bado hali ilizidi kuwa mbaya na kuninyima usingizi nikiwaza nitawawafanyaje hawa watoto," anasimulia mmiliki huyo.

Anasema wakati yote hayo yanatokea tayari alikuwa na ujauzito na daktari alimshauri kutofanya shughuli yoyote mpaka atakapojifungua na alimshauri kutoruhusu mawazo kwa sababu kufanya hivyo angepoteza mtoto wake.

"Kipindi chote hicho cha ujauzito nilikuwa nimepewa 'Bed rest' kwa hiyo mzigo wote nikamwachia mume wangu ambaye huwa nasaidiana naye kusimamia."

"Kila siku hali ilivyozidi kuwa mbaya nilizidi kuwa na mawazo na kukosa usingizi kwa sababu kwa mwezi tulikuwa tunatumia Shilingi milioni mbili kwa ajili ya huduma zote za watoto pale kituoni na ilifika siku tunaamka hatuna hata shilingi na hatujui watoto watakula nini."

"Nilishindwa kujizuia kwa sababu hali ilizidi kuwa mbaya siku hadi siku, huwezi kuamini hivi ninavyozungumzana wewe nimepatwa na matatizo makubwa sana, niliugua karibu kufa, mimba imetoka, nimepoteza mtoto wangu na bado nimepata matatizo mengine makubwa ya kiafya na imetubidi tuuze kila kitu cha nyumbani tulichokuwa nacho ikiwamo kiwanja."

Anasema baada ya kuona hali imezidi kuwa ngumu, walishauriana na mume wake kufanya shughuli yoyote ambayo itawasaidia kupata hata kipato kidogo.

"Baada ya kuona hali ya maisha inazidi kuwa ngumu, ilibidi tushauriane na mume wangu tutafute kitu chochote cha kufanya hata kama cha kutuingizia kipato kidogo, na nilipopata ahueni kidogo kiafya tulianza, na sasa tunauza juisi Mbagala (Temeke, Dar es Salaam), hii inatuasaidia kupata pesa kwa ajili ya chakula cha watoto wakati tunasubiri hali itengemae huku tukiendelea kuwasiliana na wale waliokuwa wanatusaidia," anasema.

ITAENDELEA KESHO

# Wenyeviti wa zamani wabwagwa

**Na Waandishi Wetu**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi pamoja na Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara wamefanya uchaguzi wa wenyeviti, na waliokuwa wanashikilia nafasi hizo wameangushwa.

Uchaguzi huo ulisimamiwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Masasi, Shaibu Mtawa.

Akitangaza matokeo hayo, Mtawa alisema kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mshindi nafasi ya uenyekiti wa halmashauri hiyo ni Ibrahimu Chiputula ambaye ameshinda kwa kura 28, huku Diwani wa Kata ya Chiungutwa, Juma Satma, mwenyekiti aliyemaliza muda wake akipata kura 15.

Pia, alisema Diwani wa Kata ya Chiwata, Jafari Mkwanda alipata kura nne.

Alimtangaza Diwani wa Kata ya Mpeta kuwa Mwenyekiti mpya wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Alisema wajumbe waliopiga kura katika uchaguzi huo kwa halmashauri ya wilaya walikuwa 47. Vile vile, Mtawa alimtangaza mwenyekiti mpya wa Halmashauri wa Mji Masasi ambaye ni Diwani wa Kata ya Jida, Hashimu Namtumba kwa kupata kura 10, huku mwenyekiti aliyemaliza muda wake akipata kura saba na Relian Mwajombe, akiambulia sifuri.

Alisema jumla ya wajumbe waliopiga kura ni 17 na hakuna kura iliyoharibika.

Wakizungumza baada ya kumalizika uchaguzi huo, washindi wa nafasi hizo, Chiputula na Namtumba walisema wanapongeza wajumbe kwa kufanya uamuzi na wataendelea kuwa kitu kimoja katika kuongoza halmashauri hizo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Masasi, Edward Mmavele, aliwataka madiwani hao kutotengeneza makundi badala yake wawe kitu kimoja kusukuma mbele halmashauri hizo.

**PWANI**

Madiwani wateule wa CCM wamefanya uchaguzi wa wenyeviti wa halmashauri katika maeneo mbalimbali mkoani Pwani na Bagamoyo wamepitisha jina la Abdallah Usinga wa Yombo na makamu wake akiwa Abdul Chandika.

Kibaha Vijijini, Erasto Makala ameongoza kwa kupata kura 11 na Godfrey Mwafulilwa alipata kura nane huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti ikienda kwa Efransia Kadala.

Wilaya ya Kisarawe, Zuberi Kizwezwe aliongoza kwa kupata kura 16 dhidi ya Angalieni Mpendue aliyepata kura nane na nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilichukuliwa na Mohamed Lubondo.

**MUHEZA**

Madiwani 48 wa CCM wilayani Muheza wamempigia kura mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Diwani wa Kata ya Tongwe, Erasto Mhina kushinda kwa kura 32 dhidi ya mpinzani wake Diwani wa Kata ya Ngomeni, Bakari Mhando, aliyepata kura 16. Mwenyekiti wa muda wa uchaguzi huo, Zacharia Hiza alimtangaza Mhina kuwa mshindi.

Waliogombea nafasi hiyo ni Mhando, Diwani wa Kata ya Kilulu, Fuad Rashidi na Diwani wa Kata ya Tongwe, Mhina.

**TARIME**

Uchaguzi wa kuwapata wagombea uenyeviti wa Halmasahuri ya Tarime Mjini na Tarime Vijijini ndani ya CCM umeahirishwa kutokana na majina ya madiwani wawili wa viti maalumu, Rhobi Mwita na Doris Magaiwa, kuchanganywa majina.

Akizungumza na madiwani zaidi ya 40 na wabunge wa majimbo ya Tarime Mjini, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Tarime, Daud Ngicho, alisema uchaguzi huo umeshindwa kufanyika jana kutokana na kuwapo na mkanganyiko wa majina ya madiwani wawili wa viti maalum na kupelekwa Halmashauri ya Tarime Vijijini.

"Suala hili tumelipeleka mkoani na kwa Katibu Mkuu wa CCM na uamuzi tumeletewa na kupigiwa simu kutoka makao makuu ya chama kuwa tuahirishe uchaguzi huu mpaka mkanganyiko huo utakapofanyiwa kazi ili uchaguzi ufanyike kwa uhuru na haki," Ngicho.

***Imeandikwa na Hamis Nasri (MASASI), Julieth Mkireri (KIBAHA), Steve William (MUHEZA) na Samson Chacha (TARIME)***



Diwani wa Kata ya Tongwe, wilayani Muheza mkoani Tanga (CCM), Erasto Mhina (katikati), akiwa na Katibu wa CCM Wilaya hiyo, Mohamed Moyo (kushoto) na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA', baada ya kuchaguliwa na chama hicho, kuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hakimu atoa somo taratibu kukiri kosa kwa DPP

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imesema jukumu la washtakiwa wenye nia ya kukiri makosa na kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) ni kufuata utaratibu sahihi badala ya kutaka majibu ya maombi yao mahakamani.

Hakimu Mkazi Mkuu, Kassian Matembele, alisema jana wakati kesi ya kutakatisha Sh. bilioni 1.477 inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kulthum Mansoor, ilipopangwa kutajwa.

Kesi hiyo ilitajwa jana kwa njia ya mahakama mtandao.

Hakimu Matembele alisema utaratibu wa kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano ni kati ya mshtakiwa au ndugu na Ofisi ya DPP hivyo inawapaswa kufuata utaratibu sahihi wa kufuatili katika ofisi ya DPP mpaka wanapopata majibu badala ya kwenda kuuliza majibu mahakamani.

"Siyo kazi ya mahakama kufuatilia hilo, mahakama inahusika tu pale ambapo mmeshafikia makubaliano ndipo inahusika katika utekelezaji wa makubaliano," alisema.

Awali, Wakili wa Serikali, Wankyo Simon, alidai shauri hilo lilikwenda mahakamani hapo kwa ajili ya kutajwa, lakini upelelezi bado na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya kutoa hoja hiyo upande wa utetezi katika kesi hiyo uliomba upande wa mashtaka kuharakisha upelelezi huku akieleza maombi ya kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano na DPP ilipofikia.

Kupitia Wakili wa Utetezi, Elia Mwingira, alisema haoni ushirikiano wala maendeleo yoyote katika suala la kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano huku akisema kuwa ofisi ya DPP iliwaambia watapata majibu kutoka kwa ofisi ya mawakili, lakini mpaka sasa hajapata majibu kamili.

Akijibu hoja hiyo, Wankyo alidai kuwa upande wa utetezi unaendelee kufuatilia na kuwataka wasikate tamaa pamoja na kuwa upelelezi haujakamilika watajitahidi kuharakisha.

Katika kesi ya msingi Kulthum anakabiliwa na mashtaka manane likiwamo la kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha kiashi cha Sh. 1,477,243,000.

# DC aeleza chanzo moto uliounguza bweni

**Na Waandishi Wetu, MWANZA**

SIKU moja baada ya kutokea ajali ya moto uliounguza bweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Loreta ya jijini Mwanza, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk. Severine Mathias, amesema chanzo cha moto huo ni hitilafu ya umeme.

Kutokana na hali hiyo, amezitaka taasisi mbalimbali kufuata ushauri wa wataalamu wakati wa kujenga majengo makubwa.

Alitoa kauli hiyo juzi shuleni hapo wakati wa ibada maalum iliyowashirikisha wazazi, walimu, wanafunzi na viongozi wengine wa serikali.

Alisema tukio hilo ni baya na linasikitisha, lakini bahati nzuri hakuna mwanafunzi aliyepoteza maisha katika ajali hiyo ambayo ilitokea Jumamosi usiku.

Mkuu huyo wa Wilaya aliomba shule zote za bweni na taasisi zinazohudumia wananchi kujenga kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa zimamoto na uokoaji ili kuepusha majanga ya moto yanayojitokeza.

Alisema kwa kuzingatia maelekezo ya zimamoto na uokoaji kila jengo lizingatie tahadhari katika kujenga majengo na miundombinu inayokidhi mahitaji pamoja na vifaa vya kudhibiti na kuzimia moto ili kuepusha athari.

Alisema chanzo cha moto katika bweni hilo la ghorofa tatu ni hitilafu ya umeme kama alivyoelezwa na wataalamu wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Aliwaomba wazazi wenye watoto wanaosoma katika shule hiyo kuwa na amani kwani hakuna madhara ya kifo yaliyotokea, hivyo wanamshukuru Mungu kwani wakati unatokea moto huo ni wakati watoto walikuwa wanajiandaa kupata chakula, sala kwa kuzingatia ratiba ya shule hiyo ni ya kidini.

Aliziomba taasisi za serikali, binafsi na jamii kwa ujumla kuchangia vitu mbalimbali vitakavyowezesha wanafunzi kusoma na kurudi katika hali ya kawaida ambapo kama halmashauri itachangia baada ya tathmini kufanyika na kujua mahitaji yanayohitajika.

Pina Kiwia, mmoja wa wazazi akizungumza na Nipashe, alisema walivyopata taarifa za kuungua shuleni hapo, walipatwa na mshtuko mkubwa ambao uliwapa hofu ya kuwapoteza watoto wao ama kujeruhiwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Pastry Massota, alishukuru Mungu kwa kuwanusuru wanafunzi hao na kwamba wanapaswa kusahau yote yaliyopita kwa kuwa kesho wale wa kidato cha nne wanaanza mitihani yao.

Mmoja wa wanafunzi aliyenusurika katika tukio hilo, Abigael Vincent, alisema baada ya kuuona moto alishuka kwa uharaka chini na kutoa taarifa za moto, hivyo wanamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwanusuru na janga hilo.

Kwa upande Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angeline Mabula, alisema matukio kama hayo mara nyingi yanaumiza watoto, wanajeruhiwa au kupoteza maisha.

Aliupongeza uongozi wa shule hiyo, maana ulikuwa umejiandaa kwa tahadhari ya moto kwani ni miezi michache tu walikuwa wamekaguliwa na zimamoto, hivyo alishauri tahadhari iendelee kuchukuliwa hasa kwenye maeneo ambayo wanakuwapo watoto ili kudhibiti majanga hayo ambayo yanaweza kutokea.

**Imeandikwa na Neema Emanuel na Antony Gervas, MWANZA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera EU kwa kuonyesha njia

MWISHONI mwa wiki, mabalozi wa nchi za Umoja wa Ulaya (EU), walizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili dhidi ya wanawake yanayoanza Novemba 25 na kufika kilele Desemba 10, mwaka huu.

Mabalozi hao wa nchi za Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Uholanzi, Mkuu wa EU nchini, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN Women) na Taasisi ya Kijamii ya Tanzania Community Initiatives (TACCI).

Katika mkutano huo walieleza kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kupambana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, huku kila ubalozi ukiwa na shughuli ya kijamii itakayofanya katika siku zote 16, ambazo moja kwa moja zinaishirikisha jamii na kuwafikia wengi kwa wakati mmoja.

Kila balozi na mkuu wa taasisi alieleza mipango ya baadaye na uwajibikaji wa nchi yake pamoja na shughuli walizofanya na watakazofanya, ikiwa ni miradi mbalimbali ambayo ina matokeo chanya kwa wasichana, wanawake na watoto.

Mabalozi hao walisema bado hakuna usawa wa kiuchumi hasa katika sekta isiyo rasmi kwa kuwa bado asilimia 81 ya wanaume ndiyo wanapata kipato cha wastani wa Sh. milioni 1.5, huku wanawake asilimia 15 wakipata kipato hicho.

Walisema ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo la dunia na bado wanawake na wasichana wanapitia unyanyasaji wa kingono, ukatili wa kijinsia, tamaduni kandamizi.

Wanasema ili kukabiliana na yote hayo kila mwanajamii ana wajibu wa kukataa na kufikiri kama ni yeye anatendewa yote hayo, na huku kukiwa na kampeni kwenye mitandao ya kijamii kuhamasisha jamii kutokukubaliana na ukatili.

Kila ubalozi na taasisi ulitoa hakikisho lake la kuendelea kutoa fedha kwenye miradi ya wanawake, na kuhusisha wanaume ambao ni sehemu ya suluhisho, lengo kuu likiwa ni kupunguza au kumaliza kabisa ukatili dhidi ya wanawake na kuweka usawa wa kiuchumi.

Mabalozi hao wanasema ni lazima wanaume na wavulana kushirikishwa katika kupigania usawa wa jinisia kwa kuwa usawa ni wa manufaa kwa jinsi zote.

Mathalani, Ubalozi wa Ufaransa, Ubelgiji na TACCI utakuwa na shughuli za kijamii kama sherehe ya jioni kujadili ukatili wa kijinsia kwa kauli ya ninasimama kupinga ukatili katika mfumo wa taaluma.

Hafla hiyo itajumuisha michezo mbalimbali kama ngoma za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuhusu unyanyasaji kingono, nafasi ya wanawake katika ngazi ya maamuzi na ndoa za utotoni.

Pia, mabalozi hao watakuwa na burudani ya wazi ikiwa na kauli mbiu ya usiku wa kuwawezesha wanawake kujieleza wenyewe na kupata nafasi mbalimbali katika ngazi zote.

Ubalozi wa Uholanzi watakuwa na filamu ya Nigeria kuhusu unyanyasaji wa kingono.

Tunazipongeza balozi hizi kwa hatua kubwa ya kushiriki kikamilifu kwa mambo yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja, kwa kuwa miradi hiyo itanufaisha wanawake moja kwa moja.

Tunawapongeza kwa kuisaidia jamii ya Watanzania, kwa kuhakikisha mila potofu kama ndoa za utotoni, ukeketaji na ukatili dhidi ya wanawake unakomeshwa.

Tunashauri ni vyema fedha za miradi ya kuwasaidia wanawake zinapopelekwa kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali, zitumike vyema na kuwafikia walengwa, ili mabadiliko yanayotarajiwa na wanaotoa fedha za walipakodi wao yafikiwe.

Maadhimisho haya yanafanyika wakati ambao kuna ongezeko la matukio ya ukatili dhidi ya wanawake, kwa kupigwa, kujeruhiwa na kuuawa na waume zao kwa sababu kama za wivu wa mapenzi na nyinginezo ambazo hazina msingi wowote wa kudhuru maisha ya binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Madudu haya elimu yasiwe sikio la kufa lisilosikia dawa

Na Sabato Kasika

WALIMU wakuu wa shule za msingi kadhaa wanatuhumiwa kufanya udanganyifu kwenye mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi na kusababisha wanafunzi 1,059 kufutiwa matokeo ya mtihani huo.

Mbali na walimu hao wa shule 38, watuhumiwa wengine wa udanganyifu ni walimu wa taaluma, mgambo na wasimamizi ambao waliandaa vikundi vilivyohusisha wahitimu wa sekondari, waliowafanyia mtihani.

Hiyo ni kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde, kwamba baadhi ya watuhumiwa wamekamatwa wakiwamo 11 kutoka Halmashauri ya Gairo na 12 wa Mvomero mkoani Morogoro.

Watuhumiwa wengine ni 13 wa shule tatu tofauti kutoka Bariadi mkoani Simiyu, huku Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora wakiwamo 11 na Halmashauri ya Moshi mkoani Kilimanjaro wapo watano.

Aidha, jijini Arusha wamenaswa watano, Halmashauri ya Tandahimba mkoani Mtwara saba, na ya Kiteto huko Manyara ni wanne na Buchosa mkoani Mwanza Katibu Mkuu anasema wamenaswa watatu.

Wakati hayo yakiwa yamejiri kwenye mtihani wa darasa la saba, Dk. Msonde, anasema katika mtihani wa kidato cha nne ulioanza jana, wamebaini shule 71 ambazo ziko katika mchakato wa kufanya udanganyifu.

Ikumbukwe kuwa si mara ya kwanza kuwapo kwa maonyo na hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa kwenye udanganyifu wa mitihani kwa shule za msingi na sekondari.

Serikali imekuwa ikionya na kukemea mtindo huo wa udanganyifu na wizi kwenye mitihani kuanzia ngazi ya shule za msingi na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaobainika kujihusisha na mchezo huo.

Mwaka 2014, NECTA ilitangazia umma kuwa imedhibiti wizi wa mitihani ya taifa na udanganyifu katika ngazi mbalimbali za elimu nchini.

Mafanikio hayo yanatajwa kuwa yanatokana na ushirikiano uliopo kati ya NECTA na kamati za uendeshaji mitihani za mikoa na wilaya, ili kutatua tatizo la wizi wa mitihani ya taifa na udanganyifu.

Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala wa NECTA, Daniel Mafie, ndiye aliyetoa taarifa katika mkutano na wanahabari kuelezea mafanikio yaliyokuwa yamefikiwa na baraza hilo wakati huo.

Lakini, ajabu ni kwamba bado madudu yanaendelea kujitokeza kila mwaka, hali inayoonyesha kuwa wanaojihusisha udanganyifu huo wamekuwa ni sawa na sikio la kufa ambalo halisikii dawa.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa madudu kwenye mtihani wa taifa ni ya muda mrefu ya miaka nenda rudi ingawa serikali inajitahidi kupambana nayo, lakini bado yanaendelea kujitokeza kila mwaka.

Mfano mmojawapo ni matokeo ya mwaka 2011 ya mtihani wa darasa la saba, watahiniwa 9,736 walifutiwa matokeo kwa kufanya udanganyifu, huku mwaka 2013, 272 wa kidato cha nne nao wakifutiwa kwa kosa hilo.

Ni vyema kukumbushana kuwa, udanganyifu katika mitihani una mchango wa kuporomosha elimu hivyo wahusika wanatakiwa kulitambua hilo na kuachana nalo.

Udanganyifu na wizi wa mitihani huzalisha wasomi wasio na manufaa kwa taifa, hivyo upigwe vita na wadau wa elimu na pia wahusika waendelee kuchukuliwa hatua za kisheria.

Haipendezi kufaulu kwa udanganyifu na kuchaguliwa kwenda shule ya vipaji maalum wakati hana sifa jambo linaloweza kurudisha nyuma maendeleo ya elimu.

Wanaofanya mchezo huo huenda wanafahamu madhara yanayotokana na udanganyifu huo, hivyo ni vyema kuachana na mambo hayo yasiyo na tija kwa taifa.

Watambue kuwa, udanganyifu na wizi wa mitihani ni vitendo vyenye athari kuanzia kwa wanafunzi, walimu shule na taifa kwani ni kukwamisha hatima ya elimu.

Inasikitisha kuona wenye wajibu wa kusimamia kanuni na weledi katika mitihani, ndiyo wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo hivyo viovu badala ya kuinua viwango vya ufaulu kwa wanafunzi wanabomoa.

Yaliyopita si ndwele waliopewa dhamana hiyo wabadilike ingawa inawezekana wachache ndiyo wanaowaharibia wenzao, lakini suala la msingi ni kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za kusimamia mitihani kwa weledi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (kushoto), akipokea hati ya viwanja saba na nyumba kutoka kwa mwenyekiti wa timu iliyoundwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kufuatilia mali za vyama vya ushirika, Asangy Bangu, jana, ambazo ni mali za Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga, (SHIRECU), zilizouzwa kinyume na taratibu na kuuziwa watu binafsi. Habari Uk. 2. **PICHA: MARCO MADUHU**

# JATU yapata usajili DSE

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Masoko ya Mitaji na Dhamana nchini (CMSA) imeipongeza kampuni ya 'Jenga Jumuiya Tokomeza Umaskini (JATU), kusajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na kuitaka kulinda maslahi ya wanachama wake.

Akizungumza wakati wa kuisajili kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana , Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mkama, alisema hatua hiyo itazidi kuongeza imani kwa wananchi waliojitolea kuwekeza katika kampuni hiyo.

Alisema kampuni hiyo iliyojihakikishia kutoa gawio la asilimia 30 la kila mwaka kwa wanachama wake ni suala ambalo linaonyesha wazi kuwa kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Nitaka bodi na wakurugenzi wa JATU kuhakikisha uwekezaji unakuwa wa faida kwenu pamoja na wanachama kwa ujumla, kwa kuwa ndiyo njia sahihi ya kufanya kampuni iweze kukua," alisema Mkama.

Aidha, aliwataka Watanzania kutumia fursa zilizopo katika masoko ya mitaji kuwawezesha wananchi kukua kiuchumi na kwamba kwa kufanya hivyo ni wazi watakuwa wameiunga mkono serikali katika jitihada zake za kiuchumi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya JATU, Dk. Zainuna Yonah, alisema tukio la kampuni hiyo ya wananchi kusajiliwa katika soko la hisa, linahitimisha safari ya muda mrefu kujiunga na DSE na kusisitiza kwa sasa kazi iliyobaki ni kutoa majibu ya changamoto zilizokuwa zikiwakabili.

Alisema kwa sasa baada ya kampuni hiyo kuorodheshwa katika soko la hisa, mbali na kuongeza wigo wa kushirikiana na serikali, kutawawezesha Watanzania kupiga hatua katika uchumi wao binafsi pamoja na taifa kwa ujumla na hivyo kutokomeza umaskini.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa JATU, Peter Isare, alisema kampuni hiyo inayomilikiwa na wanawake, vijana pamoja na watu wa kipato cha kati, wamejiunga pamoja na kushirikiana katika miradi mikubwa ya kilimo, viwanda, masoko na TEHAMA.

Alisema hadi kufikia mafanikio hayo ya kusajiliwa soko la hisa, wameweza kuanzisha mashamba katika hekari zipatazo 17,678 yaliyopo katika mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwamo Tanga, Manyara, Singida, Ruvuma, Morogoro na Njombe.

Alisema hatua ya kampuni hiyo kuorodheshwa katika soko la hisa kutazidi kuiwezesha kushiriki katika miradi mikubwa zaidi na hivyo kuisaidia kubadilisha maisha ya maelfu ya Watanzania.

# NCC yaalika wadau kutumia maktaba yake

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Ujenzi la Taifa (NCC), limefungua milango kwa wadau wa masuala ya ujenzi, wakiwamo makandarasi, wasanifu majengo, wakadiriaji, mafundi ujenzi wa ngazi mbalimbali na wana vyuo wa taaluma hiyo, watumie maktaba ya taasisi hiyo kujisomea mambo ya kitaaluma, ili kujiongezea maarifa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Matiko Samson Mturi, alisema hivi karibuni kuwa NCC ina vitabu visivyopatikana katika maktaba nyingine nchini na hata nje, ndio maana imekuwa ikiazimwa baadhi ya vitabu na wataalamu wanaotoka nje ya Tanzania, pamoja na taasisi za ujenzi zilizoko nje ya nchi.

Dk. Mturi alisema maktaba hiyo yenye vitabu 424, imesheheni machapisho mengine mbalimbali yenye taarifa za ukuaji na maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini, tangu miaka ya 1980.

Alisema, umefika wakati wadau wa ujenzi nchini waitumie, badala ya kuachia fursa ya kupata maarifa kupitia vitabu kwa watu na taasisi za nje.

"Ni vyema ikafahamika kuwa NCC ina maktaba inayojitosheleza kwa vitabu muhimu vinavyohitajika kwenye sekta ya ujenzi kwa sasa. Ieleweke pia kuwa baraza linaruhusu wadau mbalimbali wa masuala ya ujenzi waitumie maktaba yetu, kwa kuzingatia masharti rahisi ya muda wa kazi na kuwa na hitaji la kweli la kitabu."

Pia Dk. Mturi alisema, hakuna malipo kwa yeyote anayefika kutumia maktaba hiyo. "Hata kama itabadilika baadaye, kwa sasa ni bure kutumia maktaba ya NCC," alisema.

Alisema lengo ni kuamsha ari ya wadau wa ujenzi kujisomea na kupata maarifa ya kiufundi zaidi ambayo vitabu vilivyopo vimeyagusa moja kwa moja.

"Maktaba yetu iko ghorofa ya tisa kwenye jengo la Samora (Samora Tower) lililopo katika Mtaa wa Mansfield jijini Dar es Salaam," alisema.

Hata hivyo, alisema ni watu wachache wanaofika kupata huduma, jambo linalompa wasiwasi kwamba huenda utamaduni wa watu kutopenda kujisomea umeendelea kuwa tatizo.

Alisema watu na taasisi za nje ya Tanzania ndio wamekuwa wakivutiwa zaidi na vitabu vilivyopo katika maktaba hiyo kutokana na jinsi wanavyovichangamkia kwa kuviulizia, kuvisoma na wengine kuviazima.

"Maktaba ya NCC ni kubwa na ina wafaa pia wataalamu wanaofanya utafiti wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ujenzi. Ni vyema ikaeleweka kuwa NCC ina majukumu tofauti likiwamo la kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya ujenzi kupitia vitabu na machapisho mengine ya kitaaluma yaliyopo maktaba.

Majukumu mengine ya NCC aliyoyataja ni kutoa elimu ya usuluhishi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi, kutoa ushauri wa kiufundi katika masuala yote yanayohusiana na sekta ya ujenzi na kufanya utafiti unaohusu masuala ya ujenzi nchini.


**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS) 2020-11-23**

**WANAOCHUKUA BIDHAA ZA WAFANYABIASHARA**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linawataarifu wafanyabiashara kuwa hivi karibuni kumekuwa na watu wanaojitambulisha kuwa ni wafanyakazi/wakaguzi wa TBS na kufanya ukaguzi kwenye maduka yanayouza bidhaa za chakula na vipodozi, ikiwa ni pamoja na kukamata na kuchukua bidhaa hizo zisizoruhusiwa kuuzwa hapa nchini na kuwaagiza wafanyabiashara kufuata bidhaa hizo TBS kwa maelezo na hatua zingine za kisheria.

TBS inapenda kuwafahamisha wafanyabiashara kuwa wakaguzi wa Shirika wanapofanya ukaguzi huonesha vitambulisho kabla ya kuanza ukaguzi na hawana tabia ya kutisha wafanyabiashara na kukamata bidhaa bila ya kufuata utaratibu maalumu na wala Shirika halifanyi ukaguzi wa kukamata bidhaa feki kwani jukumu hilo ni la taasisi nyingine za Serikali.

TBS inatoa ushauri kwa mfanyabiashara yoyote pindi atakapopata mashaka na mkaguzi yoyote kufanya mawasiliano na TBS ili kujiridhisha na uhalali wa zoezi pamoja na mkaguzi husika kwa kutumia mawasiliano tajwa hapo chini

**Imetolewa na :**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Viwango Tanzania (TBS),**
**SLP 9524, Dar es Salaam.**
**Simu: +255(022)2450298/Hotline: +0800110827**
**Barua pepe: info@tbs.go.tz/Tovuti: www.tbs.go.tz**
**malalamiko @tbs.go.tz**

# Makandarasi wazawa waiangukia serikali

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, imeshauriwa kuendelea kuwaamini makandarasi wazawa kuwa wana uwezo wa kujenga kwa viwango vinavyotakiwa na kukamilisha kwa wakati kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja.

Akizungumza wakati akikagua shughuli za ujenzi wa barabara pamoja na daraja la Mto Msosa, zinavyoendelea kujengwa na mkandarasi mzawa wa kampuni ya KAGWA, Diwani Mteule wa Kata ya Ighombwe, wilayani Ikungi, Mwandu Magodi Shagembe, alisema endapo serikali itaendelea kuwaamini na kuwakabidhi kazi makandarasi wazawa itawarahisishia zaidi upatikanaji wao kutakapotokea changamoto yeyote kwenye miundombinu hiyo.

"Tunaishukuru serikali kwa kumpatia mkandarasi mzawa kazi hii ya kujenga daraja kubwa kama hili, tulikuwa hatujawahi kuona kwani tumezoea kuwaona makandarasi kutoka China, Ujerumani lakini Tanzania sana sana makandarasi wa Kichina walikuwa wanajenga madaraja, lakini kwa serikali hii imeanza kuwaamini makandarasi wazawa," alisisitiza.

Aidha, alisisitiza pia kwamba endapo serikali itaendelea kuwaamini na kuwakabidhi kazi makandarasi wazawa itakuwa rahisi zaidi kuwapata kunapotokea changamoto yoyote kwenye miundombinu hiyo anapohitajika kwenye eneo lake la kazi, tofauti ilivyo sasa wanapokabidhiwa Wachina.

"Serikali iendelee kuwaamini makandarasi hawa wazawa, ili waendelee kutusimamia ujenzi wetu kwa sababu wanakuwa karibu na sisi, na inakuwa ni rahisi pia hata tunapoona barabara imekatika ni rahisi kuwaita na kufika kwenye eneo la tukio na kutengeneza vizuri," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Shagembe, daraja la Mto Msosa limejengwa kwa kiwango kizuri sana na linaonekana kuwa ni daraja zuri na limejengwa na makandarasi wazawa ambao ni wananchi wa hapa hapa Tanzania.

"Kwa hiyo tunaendelea kuomba Rais wetu aendelee kuwaamini na kuwapa kipaumbele wazawa waendelee kusimamia miradi yetu inayojengwa kwa fedha za walipakodi wenyewe," alifafanua zaidi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ighombwe, Iren Bakari, alisema kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo kutasaidia kuondokana na changamoto zilizokuwa zikiwakabili zaidi ya wananchi 19,000 wa kata za Iyumbu, Mgungira pamoja na Ighombwe wanaolitumia daraja hilo.

"Tunaishukuru serikali ilikuwa ni adha kubwa kwa sababu mvua ikinyesha haijalishi mvua imenyesha wapi, haijalishi iwe imenyesha Singida mjini au iwe imenyesha huku, hadha ilikuwa ni kubwa sana kwa mto kujaa," aliweka bayana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ujenzi ya KAGWA yenye makao yake makuu mjini Singida, Janes Ezra, alisisitiza kwamba kazi hiyo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni moja inatarajia kukamilika kabla ya wakati uliopo katika mkataba.

"Hii kazi mkataba wetu ni siku 240, lakini mpaka sasa hivi tumefikia asilimia 95 tuna siku 88, au tuseme kama siku 90 kwa hiyo tupo ndani ya wakati maana mkataba wetu unatakiwa uishe Aprili, mwakani, lakini ndani ya siku saba zijazo tutakuwa tumemaliza kazi yetu na kuikabidhi serikali," alisema.

Samweli Moleli, dereva wa magari makubwa yaliyokuwa yakitumia barabara pamoja na daraja hilo la Mto Msosa, alisema awali barabara hiyo haikuwa ya kuridhisha na kwamba kwa sasa inapitika.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Butata, Kata ya Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakijisomea katika maktaba mpya ya shule hiyo, mwishoni mwa wiki, ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi, mbunge na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (PCI). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jiji la Arusha kinara mtihani darasa la 7

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imekuwa mshindi wa kwanza kwa kuzibwaga halmashauri nyingine 184 katika mtihani wa darasa la saba uliofanyika mwaka huu.

Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. John Pima, alisema pia jiji hili limeshika nafasi hiyo kwa miaka mitatu mfululizo pamoja na mwaka huu 2020.

Dk. Pima alikuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, ambapo aliwapongeza walimu na watendaji wa elimu katika jiji lake kwamba kwa mafanikio hayo ni ya kujipongeza na kupongezwa na kila mpenda mafanikio na maendeleo.

"Tumefaulu kwa wastani wa 98.24 ambao ni mkubwa sana kwa mwanafunzi mmoja mmoja," alisema.

Dk. Pima alichukua fursa hiyo kuwapongeza walimu, wazazi na watendaji wa elimu katika Jiji la Arusha ambao kwa ushirikiano wa pamoja wamefanikisha ushindi huo ambao ni wakila mmoja wao.

Bila kufafanua idadi ya shule, Dk. Pima alisema zaidi ya wanafunzi 11,200 walifanya mtihani mwishoni mwa Septemba ambapo wadau wa elimu walihakikisha wameandaliwa vizuri kukabiliana na mtihani huo.

Alisema alishaweka mikakati na walimu wa shule za msingi kwamba wakifuta 0 na F kutakuwa na zawadi, lakini kwa mwanafunzi atakayepata A katika mitihani ya kitaifa mwalimu anapata shilingi 10,000.

Vilevile, alitahadharisha walimu au yoyote anayetaka kufanya udanganyifu katika mtihani wa kidato cha nne ulionza leo kuacha mara moja tabia hiyo kwani atawachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria zilizopo.

"Udanganyifu ni hasara kwa nchi maana utasababisha wataalamu ambao hawajaiva katika taaluma kwani hata katika utendaji maofisini watafanya pia udanganyifu, nawaasa tuwe waadilifu ambao utaleta ubora wa elimu katika taifa letu," alisema.

Alisema kwa mtihani wa kidato cha nne maandalizi yamekamilika ikiwamo vifaa vyote vinavyohitajika kufanyia mtihani na ulianza jana.

## Bil. 5.4/- kujenga barabara za TARURA

**Na Vincent Tiganya, TABORA**

JUMLA ya Sh. bilioni 5.4 zinatarajiwa kutumika katika ukarabati na kutengeneza barabara za Mkoa wa Tabora ambazo ziko chini ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati wa kusaini mikataba ya ujenzi na ukarabati wa barabara kwa makandarasi na TARURA.

Alisema kiasi hicho ni awamu ya kwanza ya kiasi cha Sh. bilioni 7.1 iliyoidhinishiwa TARURA kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Dk. Sengati alisema kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa kilomita 2.76 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa makaravati zaidi ya mistari 59 na uchongaji wa barabara zaidi ya kilomita 541.

Aliwasihi makandarasi 34 walioshinda zabuni ya kutengeneza na kukarabati barabara hizo kufanyakazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo, ubunifu na weledi ili serikali iendelee kuwa na imani nao na kuwapa kazi zaidi.

"Makandarasi waliomba kazi ni wengi, lakini 34 tu ndio mmefanikiwa kupata nafasi, kwa hiyo msituangashe... tangulizeni mbele uzalendo kwa maslahi mapana ya Mkoa wa Tabora na taifa kwa ujumla," alisisitiza.

Aliwataka makandarasi walioshinda zanini ya kazi hiyo kuhakikisha kazi inakamilika katika muda uliopangwa, na kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha iliyotolewa na serikali.

Aidha, alimwagiza Mratibu wa TARURA na wataalamu wake kuhakikisha wanasimamia kwa karibu miradi yote iliyopangwa ili ikamilike kwa viwango.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa miradi ya barabara, hivyo haitasita kumchukulia hatua mtumishi ambaye atasababisha miradi kutekelezwa chini ya kiwango, kwa kushindwa kusimamia majukumu yake ipasavyo.

Dk. Sengati alisema ujenzi wa miundombinu hiyo na mingine itachochea maendeleo katika sekta za utalii, kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda na biashara.

## NEMC yafunguka mradi wa umeme

**Na Mwandishi Wetu, RUFIJI**

WAJUMBE wa Bodi na Menejimenti ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wameeleza kuridhishwa na hatua za ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa majini katika Mto Rufiji wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) unavyoendelea sambamba na kuzingatia tathmini ya athari za mazingira (EIA).

Akizungumza baada ya kufanya ziara ya kutembelea mradi huo mkubwa, Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnati Chaggu, alisema baraza limejionea maendeleo ya mradi huo na hali ya uzingatiaji wa kanuni za kimazingira vinavyofuatwa na wadau wote wanaoshiriki katika ujenzi.

"Baraza lipo karibu na mradi kuhakikisha maendeleo ya mradi huo unafuata kanuni na sheria za utunzaji wa mazingira," alisema Prof. Chaggu na kuongezea kuwa ikolojia ya eneo lote la mradi linapaswa kutunza na kulindwa ili lisiathirike na shughuli za ujenzi zinazoendelea.

Aliongezea kuwa kukamilika kwa mradi huu utachochea pia utalii nchini kutokana mwonekano wa miundombinu itakayojengwa itavutia watalii, uwekezaji katika hoteli za kitalii katika maeneo ya karibu hali itakayochochea zaidi ukuaji wa uchumi nchini.

"Mradi huo unategemea zaidi utunzaji wa vyanzo vya maji vinavyopeleka maji katika Mto Rufiji hivyo ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha anatunza na kulinda vyanzo vyote vya maji na kuufanya mradi kuendelea kuwapo," alisema Prof. Chaggu.

Aidha, NEMC itaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji, ambapo ndio chanzo za kujaza maji katika bwawa linalojengwa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme Mto Rufiji.

Mradi huo unategemea zaidi utunzaji wa vyanzo vya maji vinavyopeleka maji katika huo, hivyo kila Mtanzania kuhakikisha anatunza na kulinda vyanzo vyote vya maji muhimu na NEMC itaendelea kutoa elimu juu ya kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji, alisema Prof. Chaggu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema tumekuja kukagua ujenzi wa mradi ikiwa ni sehemu ya majukumu yetu katika kuhakikisha miradi ya serikali ya awamu ya tano inatekelezeka kwa vitendo kwa kila mtendaji kuwajibika katika nafasi yake.

"Kama baraza tutaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kutoa utaalamu wetu kwenye mambo ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira ili mradi huu uweze kukamilika na kuishi kwa muda mrefu pasipo kuleta athari katika mazingira," alisema Dk. Gwamaka.

Aliongezea kuwa umeme utakaozalishwa hapa megawati 2,115 utaiweka Tanzania katika ramani ya dunia kwa kuwa na umeme wa uhakika hali itakayochochea ukuaji na maendeleo katika sekta ya viwanda nchini.

# RAS awataka waajiri kuweka mifumo kulinda wafanyakazi

**Mwandishi Wetu**

KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, amewataka waajiri mkoani humo kuweka mifumo madhubuti kuwalinda wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali katika maeneo yao ya kazi.

Alisema uwapo wa mifumo mizuri maeneo ya kazi kutasaidia kuwakinga wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali zinazotokea maeneo ya kazi.

Kauli hiyo aliitoa jijini Arusha kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum ya Vision Zero yaliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA) jijini Arusha.

Alisema wafanyakazi nikipuri namba moja kwa taasisi au kampuni yeyote katika ufanisi wa kazi yeyote na wana mchango mkubwa sehemu ya kazi, hivyo hawana budi kuhakikisha wanawalindwa dhidi ya magonjwa na ajali zinazoweza kutokea sehemu za kazi ili kuwawezesha kufikia malengo waliojiwekea.

Katibu Tawala huyo aliwataka waajiri kutoa ushirikiano kwa OSHA, ili kuhakikisha suala hilo linatekelezwa bila vikwazo, kwani wafanyakazi ndio watendaji wa kazi, endapo ushirikiano utakuwapo baina yao, itasaidia kupunguza ajali na magonjwa sehemu za kazi.

"Suala hili ni la pande tatu yaani mwajiri, mwajiriwa na serikali na endapo ushirikiano huo utadumishwa basi ajali na magonjwa yatapungua ama kuisha kabisa sehemu za kazi," alisema Kwitega.

Hata hivyo, aliwataka wafanyakazi kujenga utamaduni wa kujilinda wenyewe wakiwa kazini, kwani wao wanabeba jukumu kubwa la kujilinda dhidi ya magonjwa na ajali sehemu za kazi. Kwa upande wake Mkurugenzi wa Usalama na Afya OSHA, Mhandisi Alex Ngata, alisema, Kampeni ya Vision Zero ni ya kidunia, kwani nchi mbalimbali dunia zinatekeleza kampeni hiyo huku lengo kuu la Vision Zero likiwa ni kupunguza ajali na magonjwa sehemu za kazi.

Mhandisi Ngata alisema uwapo wa mfumo sehemu za kazi utawawezesha waajiri kujikagua wenyewe, na hivyo kuweza kuzuia magonjwa na ajali sehemu za kazi.

"Mfanyakazi ni msingi imara katika biashara na uzalishaji ambao OSHA unaungalia bila wao hawawezi kuzalishana kufanyabiashara hivyo ni muhimu kuzingatia usalama na afya zao wakiwa kazini na kuwapo mfumo wa kulinda nguvu kazi hiyo," alisema Mhandisi Ngata.

Washiriki wa mafunzo hayo kwa nyakati tofauti walisema, Vision Zero itawasaidia kuweka mifumo mizuri ya kuwalinda wafanyakazi juu ya ajali na magonjwa sehemu za kazi.

"Kama mwajiri atatekeleza kama ambavyo Vision Zero inataka, kuondoa magonjwa na ajali sehemu za kazi na kama utafuata maelekezo, natumaini tutazalisha sana sehemu za kazi na hivyo kuongeza pato la taifa na ukisema umeondoa ajali na magonjwa sehemu za kazi, hata wafanyakazi watakuwa na moyo wakufanyakazi zaidi na pia watakuwa nguvu za kufanyakazi zaidi, tutawashawishi waajiri wetu watekeleze kama ambavyo lengo kubwa la Vision Zero linataka," alisema Emmanuel Mvamila, mwakilishi wa kiwanda cha TPC Moshi.

Vision Zero ni kampeni ya kidunia ambayo inatekelezwa kwenye mataifa mbalimbali duniani, kampeni hiyo ilianzishwa kwa lengo la kupunguza ajali na magonjwa sehemu za kazi, kampeni hiyo inataka maeneo ya kazi kuwekwa mifumo ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali sehemu za kazi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (mwenye miwani), akizindua kampeni za upandikizaji wa mimba kwenye ng'ombe wa kienyeji katika Kata ya Bugwema Wilaya ya Musoma mkoani Mara juzi, kwa lengo la kuongeza ubora na wingi wa mifugo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wafugaji watakiwa ushirikiano kufanikisha mkakati ufugaji kisasa

**Na Sabato Kasika**

WAFUGAJI wametakiwa kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ili kufanikisha mkakati wa miradi ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe bora wa maziwa na nyama laini na ngozi nzuri kwa ajili ya soko la uhakika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabliel, ndiye aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizindua kampeni ya uhimilishaji wa ng'ombe katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara.

Uhimilishaji huo ulifanyika Kata ya Bugwema na kuhudhuriwa na viongozi wa wilaya hiyo, wafugaji, wawakilishi kutoka ofisi ya mbunge wa Musoma Vijijini na wadau wengine wa sekta ya mifugo.

Prof. Ole Gabriel alisema, lengo la uhimilishaji huo ni upandikizaji kwa kuweka mimba kwenye ng'ombe wa kienyeji kwa kuweka mbegu za ng'ombe wa kisasa kwa njia ya mrija ili kuongeza ubora na wingi wa mifugo.

"Wafugaji toeni ushirikiano kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuanzisha miradi ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe bora wa maziwa na nyama laini na ngozi nzuri kwa ajili ya soko la uhakika," Prof. Ole Gabriel alisema.

Alisema ni muhimu wafugaji kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali ili kuachana na ufugaji wa mazoea, badala yake watoe ushirikiano ili kufanikisha mpango huo wa uhimilishaji.

"Kuwa na ng'ombe ni utajiri, hivyo wafugaji wanatakiwa kuwa tayari kuzingatia maelekezo ya serikali, kwa kuwa ina lengo la kuwasaidia kunufaika na utajiri wa mifugo walionayo," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, alisema, ofisi yake kwa kushirikiana na idara ya mifugo, watafanyia kazi kilichosemwa na katibu huyo, kwa kuhimiza wafugaji kufuata maelekezo ya serikali.

"Kwa niaba ya wakazi Wilaya ya Musoma wakiwamo wafugaji, tunakushuru na tunaahidi kufuata maelekezo ulioyatoa kwa wafugaji kwa kuwahimiza waendelee kuyazingatia ili wanufaike," alisema Dk. Anney.

Alisema, Kata ya Bugwema ni miongoni mwa kata 21 za wilaya hiyo yenye wafugaji wengi wa ng'ombe na kwamba ndiyo maana uhimilishaji umefanyika eneo hilo.

# Upelelezi ukuta kudondokea wanafunzi wakwama

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala, jijini Dar es Salaam, limesema upelelezi wa tukio la wanafunzi kufa baada ya kudondokewa na ukuta katika shule ya watoto wadogo 'Joy Unit Daycare', haujakamilika, hadi atakapopatikana mwenye ukuta ulioanguka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala, Janeth Magomi, aliiambia Nipashe jana kuwa mmiliki wa nyumba ambayo ukuta wake ulisababisha maafa hayo, bado hajapatikana.

"Upelelezi haujakamilika kwa sababu mtu anasomeka yupo Mwanza, bado hatujampata tunaendelea kumtafuta mwenye ukuta," alisema Kamanda Magomi.

Mmiliki wa shule hiyo, Atuganile Mbosolelo, mwishoni mwa wiki alikuwa anashikiliwa na jeshi hilo, akituhumiwa kumiliki shule, bila kibali.

Jeshi hilo lilisema, walibaini mmiliki huyo anatoa huduma hiyo ya elimu bila kufuata kanuni na taratibu, ikiwamo kibali.

Shule hiyo iliyopo Mtaa wa Kisiwani, Kata ya Bonyokwa, Segerea, ilidondokewa na ukuta wa nyumba ya jirani na kusababisha vifo vya watoto watatu na sita kujeruhiwa.

"Mmiliki tunaye yule mama (Atuganile), tunamshikilia kwa sababu lazima tumshikilie shule yake haina kibali haitambuliwi, shule aliyoitengeneza mwenyewe.

Shule ina wanafunzi 16, lakini tunaendelea kumtafuta yule mwenye ukuta ulioangukia hilo jengo, tumemtambua kwa jina moja la Majani...tunaendelea kumtafuta," alisema Kamanda Magoni alipozungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki.

Novemba 18, mwaka huu, saa tatu asubuhi, kabla ya masomo kuanza ghafla ukuta wa shule hiyo ulianguka huku baadhi ya watoto wakitoka nje ya darasa, kwa mujibu wa Atuganile.

Atuganile, alisema shule hiyo ya awali ambayo ina miaka mitatu, aliianzisha kutokana na kuwa na taaluma hiyo na uzoefu kwenye kazi kwa takribani miaka 10. Wizara ya Elimu inawataka wanaoanzisha shule kufuata mwongozo na hatua kadhaa, ikiwamo kuthibitishwa kwa mwenye shule na meneja wa shule, maombi ya usajili na usajili wa walimu, kabla ya kuanzisha shule.



Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya Vedma, wakitoa mchanga uliojaa kwenye Mto Tegeta, ili kupanua njia ya maji katika daraja la Goba, barabara ya Madale, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Jamii yaaswa mila kandamizi dhidi ya watoto wa kike

**Na Richard Makore, MWANZA**

MKURUGENZI wa Shirika la Compassion International (T), Mary Lema, ameitaka jamii kuachana na mila kandamizi kwa watoto wa kike.

Akizungumza katika kongamano la wachungaji wa makanisa ya kiinjili kutoka mikoa minne ya Kanda ya Ziwa, alisema mila hizo zinarudisha nyuma maendeleo ya mtoto wa kike.

Wachungaji hao wanatoka mikoa ya Geita, Mara, Kagera na Mwanza.

Alisema wachungaji hao kutoka makanisa ya kiinjili, wanatoa huduma za kiroho, elimu na afya kwa watoto wote bila kujali jinsia.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanatoa huduma kwa watoto katika mikoa 21 na kwamba lengo lao wanataka kufikia mikoa mingine iliyobaki.

Kwa upande wake, Mchungaji wa Kanisa la Free Pentecostal Church Lumumba lililopo mji wa Chato, Reuben Mahugi, alishauri jamii kuwajali watoto ambao wanatoka familia maskini.

Alisema kupitia wafadhili wamesajili watoto 200 wenye umri wa miaka mitatu hadi saba ambao wazazi wao hawana uwezo Ili kuwasaidia kielimu na kiuchumi.

Mchungaji Mahugi alisema, kanisa hilo pia linajitolea kuwasaidia wazazi wa watoto hao kwa kuwawezesha kuanzisha miradi midogo.

"Wazazi wa watoto hao tunawapa fedha

## RC ataka kasi maboresho ya uwanja wa ndege

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

MAMLAKA ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Tawi la Tabora imetakiwa kuwasiliana na mkandarasi ambaye ni Kampuni ya M/S Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd(BCEG) China ili awe kuanza maboresho ya Uwanja wa Ndege wa Tabora kwa ajili ya kuuweka katika sura ya kimataifa.

Maelekezo hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati wa ziara yake ya kuona maandalizi ya ukarabari na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Tabora.

Alisema toka Oktoba mwaka huu, serikali imeshatoa Sh. bilioni 27 kwa ajili ya uboreshaji wa uwanja huo, ambapo miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni ujenzi wa jengo la abiria, maegesho ya magari na uzio wa usalama kuzunguka eneo la uwanja huo na mnara wa kuongozea ndege.

Alisema uwanja huo ni vema ukakamilika kwa wakati kwa sababu utasaidia kuinua sekta mbalimbali za uchumi ikiwamo kuvutia wawekezaji na watalii ambao wanahitaji kutembelea hifadhi za Taifa zinazopatikana mkoani Tabora.

Naye Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Tabora, Godfrey Kaaya, alisema jengo la abiria wanalilokusudia kujenga litakuwa na uwezo wa kuchukua abiria 250,000 kwa mwaka hadi kufikia mwaka 2035.

Alitaja faida nyingine ni kuongezeka kwa ndege za abiria na mizigo na kufunguka kwa Mkoa wa Tabora katika miundombinu.

## Wadau kilimo waiafiki mbolea ya Microp

**Na Mwandishi Wetu, IRINGA**

MBOLEA mpya aina ya Microp ambayo ni mahususi kwa ajili ya kuongeza mavuno zaidi kwenye mazao ya mahindi na mpunga imepokewa kwa furaha na wadau wa kilimo katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kikao cha kujadili namna ya kumsaidia mkulima wa zao la mahindi pamoja na mpunga ili ajikwamue na kilimo cha ukosefu wa mavuno zaidi shambani, walisema mbolea ya Microp inayotengenezwa na Kampuni ya Yara imekuja kuleta mageuzi makubwa kwa mkulima shambani na kuwa itamsaidia kuvuna mavuno zaidi pamoja na mazao kuwa na virutubisho aina tano tofauti ambavyo ni muhimu kwa ongezeko la tija kwenye kilimo cha zao la mahindi.

"Wakulima wetu wengi kwenye kilimo cha mahindi changamoto kubwa ni kwenye matumizi ya mbolea, ambapo wamekuwa wakitumia tu mazoea ambayo hupelekea mavuno kuwa hafifu shambani, lakini ujio wa mbolea ya Microp wakulima wataondokana na kupata mavuno machache ya gunia saba kwa hekali na kuongezeka hadi kufikia gunia 30 shambani," alisema Dk. Juliana Mwakisindo, mtafiti na Meneja wa Tari Kifurilo wilayani Mufindi.

Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Damas Lubuva, alisema kampuni ya Yara Tanzania imeonyesha mafanikio makubwa ya kuwajali wakulima kwenye wilaya hiyo baada ya kuzindua ujio wa mbolea ya Microp na kwamba kama halmashauri watashirikiana na Yara kutoa elimu ya shamba darasa kwa wakulima ili waweze kuongeza tija katika kilimo cha mkono.

"Sisi kama halmashauri tunadhani hii mbolea itakuwa na manufaa makubwa kwa wakulima wetu, tunachoahidi ni kutoa elimu kwa wakulima, maofisa ugani pamoja na vyama vya ushirika waweze kuipokea vizuri, lakini ili tupate tija na kuongeza uzalishaji wa mazao mengi shambani kwa kweli tunashauri kitu cha kuanza nacho kwa sasa ni kwenye upimaji wa afya ya udongo, inatakiwa tujue afya ya udongo wetu na ikiwezekana hata mashamba darasa ambayo tutafanyia kazi afya ya udongo ingejulikana," alisema Lubuva.


Kwa mujibu wa Meneja Biashara wa kampuni ya Yara Tanzania Nyanda za Juu Kusini, John Meshack, mbolea ya Microp imelenga kumnyanyua mkulima mdogo wa chini kuvuna mavuno mengi shambani na wanawashauri wakulima ambao wanamitaji midogo kuanza kutumia mbolea hiyo.

"Mkulima mwenye mtaji mdogo tunamshauri aanze na mbolea hii ya Microp na baadaye aende kwenye mbolea ya Yaramila otesha kwa sababu zile mbolea nyingine hatuzitoi sokoni, na hii bidhaa mpya ya mbolea tunalenga asilimia 80 ya wakulima wa mahindi na mpunga ambao uwezo wao ni mdogo tunawaletea bidhaa ambayo siyo gharama kubwa kwa ili wapate matokeo chanya kwenye kilimo hivi sasa," alisema Meshack.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 24, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## Ni utata au uhalisia gharama na viwango vya elimu nchini?

Ukurasa 13





Ukurasa 12

**Wilaya yaibua kaulimbiu 'Elimu Kwanza'**



Ukurasa 14

Wataalamu viwango, chakula dawa wajibu swali gumu ulaji 'aspartame'

ELIMU

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

# Manispaa Moro wajipanga kuinua MEMKWA kwa kiwango chake

NYENDO za harakati baada ya uhuru ilikuwa kuboresha elimu hasa ya msingi na kadri muda ulivyosonga mafanikio yalionekana.

Hata hivyo ilibainika kuwa kuna watu wazima wengi, kutokana na mifumo ya kihistoria, ukoloni na ukosefu wa fursa, wengi hawakuenda shule na serikali ilianza mikakati ya kuwaelimisha.

Ukawa mwanzo wa kuanzishwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima miaka ya 1970 iliyoratibu mafunzo hayo na kufanikisha wenye umri mkubwa kujua kusoma na kuandika kupitia programu za ngumbaru.

Katika awamu ya tatu iliyoongozwa na Rais Benjamin Mkapa, ulianzishwa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) ili kuwapa elimu watoto na vijana walioikosa.

Kwa msingi huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeombwa kuona umuhimu kuweka madarasa ya MEMKWA kwenye kila shule ya msingi yatakayowasaidia watoto wa mitaani na pia kuboresha hali ya elimu kwa watu wote nchini hasa walioikosa.

Akizungumza na Nipashe Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwere A, iliyoko Manispaa ya Morogoro Nivocavity Monyo, anasema kuna vituo vichache vya kufundisha watoto wa mitaani.

Anasema vilivyopo vingi vinamilikiwa na watu binafsi ambao wakati mwingine, wanashindwa kuviendeleza na kuacha jukumu hilo kwa shule za serikali baada ya kupitia utaratibu kisheria.

Anafafanua kuwa moja ya darasa la kituo cha watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kinachomilikiwa na Faraja kimelazimika kusimamiwa na Shule ya Mwere A kwa miaka miwili mfululizo baada ya mmiliki kushindwa kukiendesha.



Wanafunzi wa Morogoro wakiwa masomoni. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Mwalimu Monyo anasema kuna sababu za kuwapa watoto wa mitaani elimu na misaada mbalimbali kupitia serikali za mitaa na madarasa hayo yatafanikisha fursa hiyo ambayo wengi wanaikosa.

Anasema wanaingia kwenye vituo wakiwa na miaka tisa hadi 14, jambo linalowapa ugumu wa kuwasaidia hasa wale waliofikia umri huo mkubwa.

Kuna utaratibu unaopaswa kufuatwa, hasa jamii kutambua kuwa watoto wa miaka tisa ndiyo hupokelewa kwenye vituo hivyo, ili kuwasaidia kusoma na kupata muda wa kufanya mtihani wa darasa la nne na kuendelea na masomo, lakini walozidi umri inakuwa changamoto, anaeeleza.

Mwalimu Monyo anasema, idadi kubwa ya watoto wanaosoma kwenye kituo cha Faraja kwa sasa ni wale ambao wazazi na walezi hawana uwezo wa kuwasomesha wala kuwapa chakula kutokana na hali hiyo, wengine walishindwa kuvumilia na kuingia mitaani kuomba ili kujikimu.

Hivyo Monyo, anaiomba serikali kujenga madarasa hayo mawili sanjari na kutoa huduma za chakula, mavazi na madaftari kwa watoto hao jambo ambalo litawafanya kuwa na uhakika wa kusoma licha ya wazazi na walezi kushindwa kuwasomesha.

"Watoto wa mitaani wanahitaji kuhamasishwa ili waweze kusoma na ikiwa watakosa baadhi ya huduma na vifaa hukata tamaa na kurejea mitaani," anasema Mwalimu Monyo.

Anaeeleza kuwa kituo hicho kinasaidia watoto kusoma na kufikia ngazi za juu kielimu baada ya kufaulu darasa la nne na kujiunga na wenzao walioanza sawa na umri wao shuleni Mwere A, ambapo mpaka sasa wapo wanaosoma sekondari za Morogoro, Kingo na SUA na wengine wapo kazini baada ya kupata astashahada na shahada katika vyuo mbalimbali.

Mwalimu wa kituo cha Faraja MEMKWA, Nora Makuga anasema kituo hicho kilianzishwa kwa ajili ya watoto waliokuwa kwenye mazingira magumu wakiwamo wa mitaani ambapo kufuatia changamoto za ukosefu wa misaada mingi shuleni hapo, watoto wa mitaani wamekuwa wakipungua kila mwaka.

Anasema Faraja ilikuwa ikitoa misaada ya chakula, mavazi na vifaa vya kujifunzia na kufundishia na iliposimama kuwahudumia wanafunzi sita (watoto wa mitaani) waliacha masomo mwaka 2019.

Makuga anasema, mwaka huu kituo hicho kilipokea wanafunzi 21 kutoka kwenye mazingira magumu wakiwamo wasichana wanne na wavulana 17 wanaoendelea na masomo.

"Tunaomba serikali irasimishe vituo hivi vionekane ni rasmi na si vya ziada sababu tutapata maprofesa, wahandisi na hata viongozi wa kiserikali iwapo tutatimiza ndoto za watoto hawa wa wanaoishi kwenye mazingira magumu na wa mitaani," anasema Makuga.

Aidha, anawaomba wadau mbalimbali kukisaidia kituo hicho cha watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu ili wapate chakula, mavazi ya shule na vifaa vya kujifunzia.

### ILIKOTOKA FARAJA

Mkurugenzi wa Faraja Trust Fund, Dk. Lucy Nkya anasema walianza kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu mwaka 1998 wakianzia na watoto 250.

Anasema baada ya kuona mwitikio mkubwa, waliomba Ofisi ya Elimu Manispaa kuwapata walimu wawili, walioanza kutoa elimu hiyo katika darasa lililopo jirani na Shule ya Msingi Mwere.

Anasema ushirikiano wa polisi, wenyeviti wa mitaa na watoto wenyewe waliongeza idadi ya wanafunzi kila mwaka na kuamua kufungua kituo kingine mwaka 2002, alichokiita Neema ya Mtoto kilichopo kata ya Chamwino, Manispaa ya Morogoro.

Nkya anasema katika kuendesha vituo hivyo viwili, walipata msaada likiwamo Kanisa la Kilutheri la Denmark na kuwapatia chakula shuleni, matibabu, sare na vifaa.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wilaya yaibuka na ‘Elimu Kwanza’

## • Majibu 2021, sekondari kibao kujengwa



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bukima wakiendelea na masomo darasani. **PICHA MTANDAO**

BAADA ya awamu ya tano kuanza kugharamia elimu kuanzia darasa la awali hadi sekondari ni hatua inayoendana na ongezeko kubwa la wanafunzi kuanzia usajili shule ya msingi hadi kuingia vyuo vikuu.

Maeneo mengi yamekumbana na ongezeko hilo na mojawapo ni Wilaya ya Musoma mkoani Mara ambayo sasa iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa shule tano za sekondari, ambazo zinatarajia kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao.

Shule hizo zinatajwa kuwa ni Bukwaya, Kigera, Nyasaungu, Ifulifu na Seka, ambazo kwa mujibu wa Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya, Majidu Karugendo, ujenzi uko hatua za mwisho, ili kupokea wanafunzi hao.

Katika mazungumzo na gazeti hili wiki iliyopita, Karugendo anasema, wilaya inaendelea na mkakati wa kuboresha elimu kwa kuongeza shule za sekondari za kata, ikitumia kaulimbiu ‘Elimu Kwanza’.

“Lengo la kaulimbiu hii ni kuhimiza wananchi kutambua umuhimu wa elimu, wachangie ujenzi wa shule ili kuhakikisha watoto wao wanapata elimu bila kutembea umbali mrefu,” anasema Karugendo.

Anaongeza kuwa Idara ya Elimu Sekondari pia ina jukumu kuhakikisha shule zake zinafanya vizuri katika mitihani ya kitaifa ili kuiwezesha wilaya hiyo kuendelea kuwa juu kitaaluma.

> “ Kwa mfano kupitia fedha za mifuko ya jimbo tumetoa mifuko 100 ya simenti mabati 108, na huo ni mchango uliokwenda Sekondari ya Kigere, lakini nimeshiriki kuchangia sekondari zote.

“Wilaya inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali hasa ya ujenzi wa madarasa kwa kushirikisha wananchi, ili kupanua wigo wa elimu kwa shule za sekondari ili pia wanafunzi wawe katika mazingira bora ya kujifunzwa na kujifunzia,” anasema.

### SHULE TANO TENA

Karugendo anawahakikishia wananchi kuwa mbali na shule hizo tano kufunguliwa Januari mwaka ujao, zitajengwa nyingine tano kuanzia mwaka 2021 lengo likiwa ni kuendelea kuboresha elimu.

Anazitaja sekondari hizo wanazotarajia kujenga kuwa ni Etaro, Makojo, Ugango, Suguti na Tegeruka, ikiwa ni mwendelezo wa kuboresha elimu wilayani mwao, kuwapunguzia wanafunzi vikwazo vya njiani.

“Vilevile, miaka mitano ijayo, tunatarajia kuongoza shule za kidato cha sita kutoka mbili zilizopo sasa hadi kufikia sita na hilo litawezekana kwani tumedhamiria kuboresha elimu,” anasema.

Anaongeza kuwa wananchi wamehamasika na sasa nguvukazi yao inatumika, ikiwamo kusomba maji, mchanga, mawe, kokoto na hata watu kuanzia miaka 18 hadi 59 kutoa fedha taslimu.

Karugendo anafafanua kuwa, wilaya hiyo ina vijiji 68, kata 21 na shule sekondari 20 za kata na mbili za binafsi na kwamba wananchi wanaendelea kushirikiana na serikali katika jitihada za kuongeza sekondari mpya.

“Ninajua penye mafanikio hapakosi matatizo, hivyo hata katika mafanikio haya, yapo matatizo machache, ambayo ni baadhi ya wananchi kutoshiriki kikamilifu ujenzi wa sekondari, lakini tunaendelea kuelimisha,” anasema.

### SEKONDARI ZA VIJIJI

Karugendo anasema, baadhi ya wanafunzi hutembea umbali mrefu kufuata elimu na kujikuta wakichelewa kufika shule ama kurudi nyumbani na wakati mwingine wanafunzi wa kike wanakutana na vikwazo vingi njiani.

Kutokana na hali hiyo, anasema baadhi ya vijiji vimejenga sekondari za vijiji vyao, ili kuwaondolea watoto kero hiyo, ambayo kwa nyakati tofauti inasababisha usumbufu kwa wanafunzi.

Anatolea mfano vijiji vya Kigera Etuma, Kakisheri na Nyasaungu kwamba wakazi wake wameshirikiana na serikali kujenga sekondari za vijiji hivyo, ambazo ni miongoni mwa zile tano zitakazofunguliwa mwaka ujao na vyote vipo kata ya Nyakatende.

Wananchi wamejenga sekondari ya pili, hivyo watoto wao watasoma huko badala ya kwenda Nyakatende Sekondari, anasema.

Anafafanua kuwa kata ya Ifulifu, inaendelea na ujenzi wa sekondari ya kata hiyo, lakini wakazi wa kijiji cha Nyasaungu kilichopo kata hiyo, wamejenga sekondari ya kijiji hicho na kwamba itafunguliwa Januari mwakani.

“Wanafunzi wa kijiji hicho kwa sasa wanasoma Nyakatende Sekondari ambako ni mbali. Yaani wanafuata elimu kata nyingine, lakini wazazi wao wanaona hakuna sababu na kwa pamoja wamejitolea kujenga sekondari ya kijiji,” anasema.

### MCHANGO WA WADAU

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, anasema, ni miongoni mwa wadau wakuu wa elimu ambaye amekuwa akihamasisha uboreshaji wa elimu na pia kutoa michango mbalimbali kuleta mabadiliko ya kielimu vijijini jimboni hapo.

“Kwa mfano kupitia fedha za mifuko ya jimbo tumetoa mifuko 100 ya sementi mabati 108, na huo ni mchango uliokwenda Sekondari ya Kigere, lakini nimeshiriki kuchangia sekondari zote,” Prof. Muhongo anasema.

Anafafanua kuwa kama mbunge anashirikiana kwa karibu na viongozi wa serikali kuhimiza wananchi kuchangia maendeleo ya elimu, kwa vile elimu ina mchango mkubwa katika maendeleo.

Anasema, ingawa wapo baadhi ambao bado ni wazito, lakini anaamini kwamba, wananchi wataelewa na kushiriki kikamilifu pamoja na wadau wengine katika uboreshaji wa elimu hasa kwa kuchangia ujenzi wa shule na kuwa na za kutosha.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Nyakatende, Marere John, anasema, kwa kushirikiana na wadau wengine ametengeneza madawati 120 kwa ajili ya wanafunzi watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza katika Sekondari ya Kigera, mwaka ujao.

## Manispaa Moro wajipanga kuinua MEMKWA kwa kiwango chake

**INATOKA UK.11**

Aidha, anasema kupitia fedha za wafadhili na kusogeza huduma ya maji kwenye Kata ya Chamwino wanapoishi watoto wa mazingira magumu kwenye vituo hivyo, pia walikusanya vikundi vya kinamama na kuwapa elimu ya ujasiriamali, waweze kukopesheka na kuendelea kujikimu kimaisha.

Anasema dhana ya kuwakusanya watoto hao kuwapa elimu ilileta maana kwa sababu wengi wa watoto hao walibadilika kutoka tabia za kikatili, ubakaji na ulawiti na uvutaji sigara na kuwa watiifu.

Mwaka 1998 hadi 2020 watoto wengi waliosoma kwenye vituo hivyo wamekuwa watu wazima wakiwamo wahandisi, wamiliki wa kampuni na walimu.

Hivyo anasema watoto wa mitaani bado wapo na wanahitaji misaada mbalimbali ikiwamo elimu ambapo kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza kwenye kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa COVID -19 wafadhili walisitisha ufadhili na kufanya yeye binafsi kuviendesha vituo hivyo kwa namna alivyoweza.

### USTAWI WA JAMII


Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Hamisa Kagambo, anasema manispaa huwakusanya watoto mitaani na kuwapeleka kwenye makao maalum, licha ya kutoroka tena na kurejea mitaani.

Anataja maeneo ya Fungafunga, Raya, Mission to the Homeless, Mehayo, Agape, Mgolole na Darul Muslim ili kutunzwa na kusaidwa.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ni utata au uhalisia gharama na viwango vya elimu nchini?



Elimu bora ni pamoja na viwango vya taaluma, lugha inayoleta uelewa na ufahamu wa mambo si ukubwa wa ada. **PICHA: MTANDAO**

KUNA jitihada miongoni mwa wazazi na walezi wenye uwezo kuhakikisha kuwa watoto wao wanasoma shule zenye elimu bora na mara nyingi ubora hupimwa kwa kuangalia Kiingereza kama lugha ya mawasiliano, ufaulu kitaifa na karo.

Pengine kuna ukweli au haupo ni suala la mzazi au mlezi katika hisia lakini la msingi ni kwamba elimu ya darasa la kwanza, au la sita ni ile ile hata shule ingekuwa inalipiwa ada ya Sh. 1,000,000 kwa muhula na zipo zinazolipwa zaidi ya hapo.

Hata hivyo, wahusika wanaamini na kufurahia kuwa wamefanya jambo la maana.

Ni wazi kuwa kinachotafutwa siyo elimu peke yake ila wazazi na walezi kujiridhisha kuwa wamempeleka mtoto kwenye shule iliyo bora zaidi au anasoma katika shule ambayo kiwango chake ni miongoni ambazo zina ubora wa ngazi hiyo.

Swali hapa ni hili ni kwa kiasi gani inawezekana wanafunzi hao wapate kitu cha ziada ikilinganishwa na waliobaki? Na kama kwa mfano katika ufaulu hali hiyo inajionyesha ipasavyo na kuna thamani halisi ya elimu na manufaa mengine kulingana na fedha zinazotolewa?.

Ukiangalia kwa mazoea au kwa kusikia kutokana na matangazo ya kila wakati ya ufaulu wa shule au mwanafunzi, kuna picha kuwa ni katika shule za msingi ambako kuna ushindani mkubwa zaidi? Wazazi na walezi wanaangalia ni shule ipi iliyo bora zaidi? Viwango vya malipo vikoje?

Kuachilia mbali shule za msingi kwenye sekondari pia kuna tofauti lakini kwa kiasi fulani zinapungua na kiwango cha hisia ya sifa kuhusiana na shule anayosoma mwanafunzi wa ngazi ya sekondari siyo kama mzazi au mlezi anavyojisikia kwa shule za msingi, hali ambayo inaleta utata kimantiki.

Suala ni kuwa kiwango cha ufaulu shule ya msingi halipewi uzito mkubwa kwa vile kinachotazamwa ni kuingia sekondari.

Kinacholeta mantiki hata hivyo ni kuwa elimu ya msingi ni nyeti kwa ukuaji wa mtoto kielimu baadaye kwani kila kitu kinamtegemea mwalimu au walimu kwa jumla na hivyo ubora wa shule unakuwa ni jambo muhimu mno.

Mwanafunzi akishafika sekondari, suala la kujisomea na upana wa kuelewa kutokana na vipaji au mwelekeo fulani kwa mfano katika michepuo ya fani za sanaa, biashara au sayansi, inaanza kuonekana na hiyo haitegemei sana anachopata darasani.

Ukiwapo msingi bora na wa kutosha kumwezesha kufikiri kuhusu tatizo fulani, inawezekana akaanza kuunda hiki au kile na kukitafutia majibu.

Ina maana kuwa wazazi na walezi hawajakosea katika kutoa gharama kubwa kwa watoto wao kupitia shule zenye sifa bora za ufundishaji au mazingira mazuri ya kusoma.

Kwa miaka mingi watoto wamekuwa wakipelekwa shule nchi za jirani ili kuwa katika mazingira ya kuongea na kuandika Kiingereza kila wakati, siyo kuongea tu darasani halafu mtoto akitoka nje anatumbukia katika Kiswahili, hivyo kufifisha uzoefu wake wa lugha.

Ni tahadhari muhimu endapo elimu hiyo itaenda hivyo muda wote hadi amalize chuo, azoee ufasaha huo.

Ndiyo hapo unakuja mkanganyiko ambao unawasibu watoto kwa kiwango fulani, kuwa wakati anaanza shule wazazi au walezi wana pesa kiasi fulani wanampeleka Shule ya Kiingereza.

Wakati hajamaliza elimu ya msingi mazingira ya kipato nyumbani yakibadilika, kwani kupata na kukosa ni majaliwa, hivyo iwe ni budi kumhamisha mtoto kuingia shule za kawaida, zinazotumia Kiswahili. Mara nyingine mtoto anapata taabu kuanza kuelewa mtiririko wa kile kinachofundishwa, kwani alishazoea maelezo tofauti sana. Yako mazingira, kama ni kutaka tu kupunguza gharama, mzazi au mlezi anamwacha mtoto katika shule ya kulipia inayotumia Kiingereza, ili asivurugwe uelewa wake kwa mtiririko huo.

Ukiangalia hali hii nyingine, unakuta kuwa tofauti mojawapo iliyopo si ubora wa elimu au ngazi yake kitaaluma na kimaisha ila aina ya mazingira ambayo mtoto anaandaliwa kuishi na kwa maana hiyo shule za msingi za kutumia Kiingereza zinamwandaa mtoto kuweza kutumia lugha hiyo wakati wote.

> Ukiwapo msingi bora na wa kutosha kumwezesha kufikiri kuhusu tatizo fulani, inawezekana akaanza kuunda hiki au kile na kukitafutia majibu.

Ni kumwandaa awe na urahisi zaidi wa kufikiri na kujieleza kwa Kiingereza kuliko Kiswahili, licha ya kuwa endapo ataingia sekondari ambayo yenye mazingira hayo ya Kiingereza ataanza kupoteza mazoea hayo ila atajimudu kuongea vyema bila tatizo.

Ndiyo tofauti na waliosoma kwa Kiswahili shule za msingi na sekondari 'Uswahilini,' ambako masomo yanafundishwa kwa Kiingereza ambacho wanafunzi wanaendana nayo.

Masomo yakiisha anakuwa kama amekombolewa, aingie kwenye mandhari yake aliyozoea na siyo kulazimishwa kuongea kimombo ambacho hakikai vizuri kichwani, anatumia maneno machache kueleza hisia alizo nazo, masomo tofauti yanakuwa na misamiati inayofahamika haraka, kwa mfano neno 'process au I mean.'

Siyo mazingira ya kumwezesha kijana asome vitabu tofauti na kujisikia vyema kwani haendani na msamiati wa kitabu, hali inayojenga utegemezi wa 'past papers,' mitihani iliyopita, kama msingi wa kujisomea kutafuta kufaulu.

Suala la kufikiri, kutatua changamoto zinazotokea na kuzieleza kwa kina linakuwa halipo, kwani kufanya hivyo lazima ujisikie vizuri katika lugha, ufuatilie kilichotangulia, ndipo uanze kujenga taswira ya kitu kingine.

Ni kushiriki mjadala, siyo kuelewa tu na kuishia katika kujibu na kufaulu mtihani.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Wataalamu viwango, chakula, dawa wajibu swali gumu ulaji 'aspartame'



Sukari yenye utamu bandia 'aspartame' inayotumiwa kutengeneza vyakula na vinywaji vya aina mbalimbali inaelezwa kuwa si salama kiafya. **PICHA: MTANDAO**

DUNIA ya sasa imejaa bidhaa zenye sukari au utamu bandia ambao huitwa aspartame. Hii ni bidhaa yenye utamu mara 200 ikilinganishwa na sukari hasa ya miwa.

Aspartame hutumiwa kuongeza utamu kwenye vyakula mfano viwandani inatumika kuzalisha vyakula hasa pipi, keki, chokleti na vinywaji kuanzia soda na juisi.

Ina majina mengine, wapo wazalishaji wanaoiita NutraSweet, Equal na Canderel. Sukari hiyo inaelezwa kuwa ina athari nyingi kiafya ikihusishwa na kansa, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu na kusahau ( alzheimer), mishtuko ya moyo, kiharusi na matatizo ya akili na kuumwa sana kichwa.

Aspartame ambayo ni bidhaa ya utamu bandia inayotumika duniani kote inapatikana katika bidhaa zaidi ya 6,000 ikiwa ni pamoja na soda zinaelezwa kuwa hazina sukari (diet) vinywaji vya kuongeza nguvu au 'eneji '.

Inazalisha pipi ngumu na laini zisizo na sukari (ya miwa); lakini imo kwenye tomato sosi 'ketchup', kwenye dawa za watoto, za vitamini na za matone.

Dunia imeshuhudia miongo kadhaa kuhusu wasiwasi wa aspartame ambayo imekuwapo na hadi leo wasomi wanaendelea kuizungumzia na ikumbukwe kuwa aspartame iliidhinishwa kwa mara ya kwanza mnamo 1974.

Hata hivyo licha ya kutumia miaka 50 sasa wanasayansi wa Marekani na wengine huru wameibua wasiwasi juu ya athari za kiafya na upungufu katika sukari hiyo.

> "Ikilinganishwa na sababu nyingine za mazingira zilizounganishwa na uvimbe wa ubongo, aspartame huchangia ongezeko la hivi karibuni la kiwango cha ugonjwa mbaya wa uvimbe wa ubongo.

Kuanzia mwaka 1987 taarifa za uchunguzi zilichapishwa zikiripoti kuhusu wasiwasi huo na changamoto za aspartame kiafya na uduni wa utafiti uliosababisha kuipa idhini ya kuitumia kama chakula cha binadamu.

Kunaripotiwa kuwa katika tathmini ya Mamlaka ya Usalama wa Chakula Ulaya, ilipendekezwa mtengenezaji maarufu wa sukari hiyo bandia duniani apigwe marufuku.

Wataalamu wa usalama wa chakula wanataka sukari hiyo yenye utamu wa bandia inayotumiwa sana duniani au aspartame kupigwa marufuku nchini Uingereza na kuhojiwa kwanini ilionekana kuwa inakubalika hapo awali.

Taarifa za Jarida la Chakula za Novemba 2020, zinasema uuzaji wa aspartame unapaswa kusimamishwa kwani ni kemikali inayotuhumiwa kutokana na utamu na imependelewa bila kufanyiwa tathmini ya usalama.

Athari za kiafya na mambo muhimu kwenye aspartame zinasema kuwa ingawa utafiti mwingine kati nyingine hazijaripoti matatizo yaliyoko kwenye aspartame utafiti uliofanywa na watafiti wa kujitegemea uliofanywa kwa miongo kadhaa umeunganisha aspartame na orodha ndefu ya bidhaa zenye changamoto za kiafya zikiitaja saratani.

Katika utafiti kamili wa saratani hadi sasa kwenye jina la aspartame, utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa Saratani ya Cesare Maltoni cha Taasisi ya Ramazzini, ulitoa ushahidi madhubuti kuwa ilisababisha saratani katika panya.

Utafiti unasema aspartame ni chanzo cha magonjwa hasa saratani kwa viumbe hai hata kama italiwa kwa kipimo cha kila siku cha kiwango kidogo kuliko ulaji unaokubalika kwa siku

Ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa kwa panya mwaka 2006, kwa mujibu wa jarida la utafiti uliofangalia afya na mazingira. Utafiti mwingine wa ufuatiliaji uliofanyika mwaka 2007 uligundua kuongezeka kwa kiwango cha juu cha tumors mbaya (vivimbe vyenye saratani) katika panya wengine.

"Matokeo yanathibitisha na kuimarisha uchunguzi wa kwanza wa majaribio ya [kansa ya aspartame] na uwezekano wa kusababisha saratani katika kiwango cha kipimo karibu na ulaji unaokubalika wa kila siku kwa wanadamu.

Wakati huo huo ilielezwa kuwa ulaji wa bidhaa hiyo yenye utamu kupindukia wakati wa ujauzito, athari zake za kansa huongezeka, watafiti waliandika.

Matokeo ya utafiti wa athari za maisha uliofanywa mwaka 2010 yalithibitisha kuwa aspartame ni chanzo cha kansa.

Watafiti wa Chuo Kikuu cha Harvard mnamo mwaka 2012 waliripoti kuwa ulaji wa aspartame na hatari kubwa ya ugonjwa wa lymphoma (kansa ya seli za kinga ya mwili) kwa wanaume wengi na leukemia kwa wanaume na wanawake.

Katika ufafanuzi mwingine uliofanyika mwaka 2014 na kuchapishwa katika Jarida la Marekani watafiti wa Kituo cha Maltoni waliandika kuwa matokeo ya hivi karibuni ya athari za maisha na kusababisha kansa kwa panya yaliyochapishwa katika majarida ni ushahidi thabiti wa uwezekano wa aspartame kuwa chanzo cha saratani.

Kwa msingi wa ushahidi wa athari zinazoweza kusababisha kansa, tathmini mpya ya msimamo wa sasa wa mashirika ya kimataifa ya udhibiti lazima izingatie suala la dharura la afya ya umma.

**VIVIMBE UBONGONI**

Mwaka 1996, watafiti waliripoti katika majarida ya mishipa ya fahamu kuwa aspartame inaongeza uwezekano wa kupata vivimbe vya saratani (tumors) ubongoni.

"Ikilinganishwa na sababu nyingine za mazingira zilizounganishwa na uvimbe wa ubongo, aspartame huchangia ongezeko la hivi karibuni la kiwango cha ugonjwa mbaya wa uvimbe wa ubongo.

Inaelezwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio ya uvimbe mbaya wa ubongo (katika miaka ya karibuni kufuatia idhini ya kutumia aspartame.

Watafiti wanasema inatosha kushuku kuwa sukari hiyo yenye utamu wa bandia inahitaji kuhakikiwa zaidi.

Uchunguzi wa mapema juu ya aspartame katika miaka ya 1970 ulipata ushahidi wa uvimbe wa ubongo katika wanyama waliokuwa wakijaribiwa maabara, lakini utafiti huo haukufuatwa.

**MARADHI YA MOYO**

Uchunguzi wa mwaka 2017 uliofanywa juu ya vitamu vya bandia na kuchapishwa katika Jarida la Canadian Medical Association, haukupata ushahidi wa kutosha wa faida za kupoteza uzito kwa kutumia vitamu vya bandia katika majaribio ya kliniki.

Aidha, hakukuwa na maelezo kuhusu kuwapo na ukweli kuwa kutumia vyakula vyenye sukari bandia na "kuongezeka kwa uzito, unene na kiwango cha juu cha kunenepa sana, shinikizo la damu, ugonjwa wa kisukari kwa watu wazima na maradhi ya moyo pamoja na mishipa.

Ni vyema kupunguza chakula na kinywaji chanye sukari hiyo bandia ikielezwa kuwa wanawake waliokunywa zaidi ya vinywaji viwili vya lishe kwa siku walikuwa na hatari kubwa ya matukio ya kupata ugonjwa wa moyo na mishipa.

**KIHARUSI, ALZHEIMER**

Watu wanaokunywa soda kila siku walikuwa karibu na uwezekano wa kupata kiharusi na shida ya akili kama wale ambao walitumia mara kila wiki au chini. Hii ni pamoja na hatari kubwa ya kiharusi cha 'ischemic,' ambacho mishipa ya damu kwenye ubongo inazuiliwa, na ugonjwa wa akili wa Alzheimer.

**MITANDAO YA AFYA**

# ‘Wanaotendewa ukatili wasiwalinde wahalifu’

**Na Augusta Njoji, MPWAPWA**

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, amewataka watu wanaofanyiwa vitendo vya ukatili kutokuwalinda wahalifu ili kukomesha ukatili kwa jamii.

Shekimweri aliyasema hayo jana kwenye kongamano la wasichana lililoandaliwa na Shirika la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) wilayani humo lililowakutanisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Alisema serikali haitasita kuendelea kuwachukulia hatua wale watakao patikana na hatia kutenda vitendo hivyo na kuwataka wanaotendewa kutowalinda wahalifu hao.

“Tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuondoa matukio ya ukatili wilayani hapa na tunatambua umuhimu na ulazima wa kushirikiana na wadau hawa ili kuondoa vitendo vya ukatili kwa ujamii,” alisema.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kujiepusha na vishawishi ambavyo husababisha wengi kukatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito.

Meneja Utekelezaji wa Miradi ya Shirika hilo, Evance Rwamuhuru, alisema kongamano hilo limetoa fursa kwa wasichana ambao walikatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito wakati wakiwa shule ili kutoa funzo kwa wasichana ambao bado wanaendelea na masomo yao.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala wilayani humo, Ofisa Tarafa Olbert Mwalyego, alisema ni muhimu wanafunzi hao wakazingatia masomo yao ili kutimiza malengo waliojiwekea.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Mount Igovu, Aveline Madanya, alibainisha kuwa miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha mimba za utotoni ni wazazi kutowapatia mahitaji watoto wao, umbali mrefu na kutokuwa na elimu juu ya masuala ya uzazi.

# Mpango wa kufuatilia kero wavuvi wadogo ‘wapikwa’

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeandaa mpango wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu na kutatua kero zinazowakabili wavuvi nchini.

Akizungumza katika kikao kazi cha kupitia mpango huo wa kitaifa jijini hapa, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Emmanuel Bulayi, alisema bado wananchi wengi wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi ni maskini.

Alisema hali hiyo haikubaliki na ni kinyume na maelekezo ya sera na miongozo mbalimbali ya maendeleo ya kitaifa ya nchi ikiwamo Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015.

“Tumeona ni vyema wadau wa sekta ya uvuvi kutoka maeneo mbalimbali kukutana kujadili na kupitisha rasimu ya mpango wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu nchini,” alisema.

Alibainisha kuwa sekta ya uvuvi inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wavuvi wadogo wapatao 202,053 na zaidi ya wananchi milioni 4.5 wanategemea shughuli zinazohusiana na uvuvi ikiwamo uchakataji na biashara ya samaki na mazao mengine.

Bulayi alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kutatua kero zinazowakabili wavuvi ikiwamo uandaaji wa mpango huo. Alisema mwongozo huo umeibua na kutoa njia ambazo zikitumika kikamilifu hali ya kiuchumi na kijamii ya wavuvi wadogo itaboresha kwa kiasi kikubwa, huku rasilimali za uvuvi zikiendelea kuvunwa kwa njia endelevu.


“Usimamizi thabiti wa mwongozo huu unaweza kupelekea kuongezeka kwa ajira, kipato, chakula na lishe na hivyo wavuvi wengi kujikwamua katika umaskini uliopitiliza,” alisema Bulayi.

Alishukuru Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa hiari na kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu katika muktadha wa chakula na kuondoa umaskini.

Aidha, alisema pamoja na mwongozo huo kuwa umepangiliwa vizuri, kama utekelezaji wake hautasimamiwa ipasavyo, hautaweza kutoa tija inayotarajiwa. Naye Mwakilishi wa FAO, Dk. Oliver Mkumbo, alisema umuhimu wa mpango kazi kwa nchi ya Tanzania uko wazi ukizingatia sekta ya uvuvi inategemewa na watu wengi kwa shughuli mbalimbali za kujipatia kipato na lishe.

“Tunatambua juhudi za serikali, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zinazotekeleza mpango huu, tunaipongeza serikali na wadau kwa kuona umuhimu wa mpango huu na ni matumaini yangu utasaidia kuleta maendeleo kwa wavuvi na jamii kwa ujumla,” alisema Mkumbo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la kusimamia mazingira nchini (EMEDO), Elitrudith Lukanga, aliipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na mpango huo na kutoa wito kwa mashirika mengine kuhakikisha wanashiriki vyema katika mchakato wa utekelezaji wa mpango huo.




Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Babylus Mashauri (kushoto), akipeana mkono na Meneja wa Benki ya NBC tawi la Bukoba, Mathias Muhangirwa, baada ya benki hiyo, kukabidhi jumla ya tani nne za saruji kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Ibosa, wilayani humo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda azitaka h/shauri, shule kupanda miti

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameshauri halmashauri na shule zote kuhakikisha zinapanda miti ya vivuli na matunda kwenye maeneo yao ili kuzuia athari za mabadiliko ya tabianchi.

Pinda alitoa ushauri huyo alipokuwa akizindua upandaji miti katika Shule ya Sekondari Msanga wilayani Chamwino ulioandaliwa na Taasisi isiyo ya Kiserikali inayojishughulisha na uhifadhi na utunzaji miti iitwayo Habari Development Association (HDA).

Alisema upandaji wa miti hiyo itasaidia kupunguza idadi ya watoto kupata utapiamlo na udumavu kutokana na kutokula chakula bora ikiwamo matunda.

“Kuwapo kwa miti ya matunda katika jamii inasaidia kupata chakula kwa ajili ya kujenga afya zao, lakini miti hiyo husaidia kuleta hewa safi, vivuli na ikiwamo kuepusha mmomonyoko wa udongo,” alisema Pinda.

Aidha, alisema endapo viongozi wa halmashauri zote na jamii wataiga mfano wa taasisi hiyo wa kupanda miti ya matunda itasaidia kupunguza udumavu wa watoto zaidi ya milioni tatu kwa mwaka kutokana na wajawazito kukosa vyakula bora.

Pinda alisema katika kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa miti na kuondoa hali ya jangwa na ukame serikali imeweka mikakati kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5, ambapo kwa mwaka 2015 mpaka 2020 miti milioni 608 ilipandwa.

“Nawapongeza hii taasisi kwa kuiunga mkono serikali upandaji miti na kuifanya Dodoma ya kijani hususani katika wilaya hii ya Chamwino ambako kuna Makao Makuu ya nchi na serikali imeweka mkakati wa kuratibu na kusimamia mamlaka za serikali ya mitaa kuendelea kuhifadhi miti,” alisema.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Selela, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Bilinith Mahenge, alisema kwa sasa Dodoma ina idadi kubwa ya watu hivyo kuna haja ya kupanda miti kwa wingi ili kupata hewa.

Akisoma risala Mratibu wa HAD, Godfrey Mbowe, alisema katika kuisaidia serikali kufanya Dodoma ya kijani mpaka kufikia 2021 taasisi imedhamiria kupanda miti 100,000.

Alisema maeneo ya kimkakati itakayopandwa miti kwenye shule za msingi na sekondari ambayo itakuwa sehemu ya kivutio cha watalii.

Aliiomba serikali kusaidia kuwarekebishia gari ambayo itatumika kusambaza maji ili kumwagilia vyema miti iliyopandwa.

# Wanaume waonywa kudhulumu urithi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa mwanaume yeyote ambaye atabainika kudhulumu mali za urithi katika familia.

Chalamila alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, wakati akihitimisha kongamano la sita la jinsia ngazi ya wilaya linaloendeshwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ambalo limefanyika kwa siku tatu katika kijiji cha Hatwelo Kata ya Ijombe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wajane, wakilalamikia kuwa unapofika wakati wa kugawana mirathi ndugu wa kiume hutumia mabavu kunyang'anya mali kwa kigezo cha jinsia kwamba mwanamke hawezi kumiliki.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza kukitokea hali hiyo ndani ya familia wanawake watoe taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe ikiwamo wahusika ambao ni wanaume kurithiwa wao.

"Baadhi ya wanaume wana mambo ya ovyo sana wamekuwa na mtazamo hasi kuhusu umiliki wa ardhi na mirathi kwa wanawake wakidai hawana sifa za kumiliki sasa naagiza," alisema na kuongeza:

"Nikisikia mahali popote mwanaume amefanya ujinga huo, tunaanza na yeye kumrithi ili aone kama ni sawa ndipo taratibu nyingine za kisheria zitafuata natamani hata afunguliwe kituo cha polisi cha peke yake ili akae huko aonje joto la jiwe."

Katika hatua nyingine, Chalamila aliwaomba wanawake kutovifumbia macho vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa kwenye ndoa zao ikiwamo vipigo, manyanyaso na kunyang'anywa mali ambazo wanachuma kwa jasho lao.

Vilevile, aliwaomba wanaume wa Mkoa wa Mbeya kuchapa kazi na kuacha tabia ya kukubali kukuelewa na wanawake ambao kwa kiasi kikubwa hufanya shughuli za ujasiriamali kuendesha maisha ya familia.

Alisema kwa mujibu wa utafiti alioufanya, asilimia kubwa ya wanaume wa mkoa huo wanapenda sana kulelewa na hutumia mabavu kuchukua fedha za wake zao na kwenye kufanya starehe na michepuko.

Alisema kitendo hicho ni cha dhuluma na ukatili wa kijinsia kwa sababu ni wajibu kwa mwanaume kubeba jukumu la kutunza na kulea familia, na kuwaomba wanawake kuachana na utumwa huo.

"Asilimia kubwa ya wanaume wa Mbeya mnapenda sana kulelewa huo ndio ukweli, nimefanya utafiti, pia nimepokea malalamiko mengi kutoka kwa wanawake ofisini kwangu... huu ni ukatili wa kijinsia, badilikeni timizeni wajibu kama baba wa familia," alisema Chalamila.

Mjumbe wa Bodi ya TGNP Mtandao, Jovitha Mlay, alisema dhana ya ukatili wa kijinsia inahitaji ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ukiwamo ushiriki mkubwa wa wanaume katika mijadala mbalimbali ya jinsia ili kutoa fursa ya wao kujifunza.

Alisema wanaume wanapaswa kushiriki kwa wingi kwenye kongamano na warsha mbalimbali zinazojadilia masuala ya jinsia ili kujifunza na kutambua wajibu wao na kuweza kuachana na vitendo vya ukatii ambavyo kwa asilimia kubwa vinasababishwa na wao.

Kwa upande wake, Rose Kimaro, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, alisema katika kongamano hilo moja ya mikakati waliyoiweka ni viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji kupewa elimu juu ya umuhimu wa upangaji bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Alisema bajeti hiyo itasaidia kuweka mambo yote ya muhimu yahusuyo genda kwa kuzingatia mahitaji ya makundi yote ikiwamo wenye ulemavu, wanawake na watoto katika masuala ya miundombinu ya barabara, maji, kilimo na ununuzi wa pedi kwa watoto wa kike shuleni.

Shakila Mayumana, Ofisa Programu TGNP Mtandao, alisema wakulima wanahitaji taarifa sahihi za mabadiliko ya tabianchi sambamba na wataalamu kutoa taarifa za utafiti kuwa ni wakati upi sahihi kwa ajili kuanza shughuli za kilimo.




Katibu wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA), Dk. Gemma Berege (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya juzi, kuhusu huduma wanazozitoa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya hususani za upasuaji wa kinywa na meno ambapo hadi sasa wagonjwa 19 wamefanyiwa upasuaji ikiwa ni maadhimisho ya miaka 40 ya chama hicho. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kutumia teknolojia ya kupukuchua mazao nafaka

**Na Grace Mwakalinga, NJOMBE**

WAKULIMA wa mazao ya nafaka wanaotoka Mikoa ya Ruvuma, Iringa na Njombe, wametakiwa kutumia teknolojia ya kupukuchua mazao kwa mashine ili kupunguza upotevu wa mazao na gharama ya kutumia idadi kubwa ya watu kupukuchua kiwango kidogo cha mazao.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Njombe, Ayoub Mndeme, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa teknolojia ya upukuchuaji wa mazao ya nafaka kwa njia ya mashine ambayo ilifanyika mkoani humo.

Alisema licha ya teknolojia hiyo kutumia watu wachache na kwa ufanisi, ina uwezo wa kupukuchua kiasi kikubwa cha nafaka kwa muda mfupi hivyo kuwafanya wakulima wengi kuvutiwa kutumia mashine hizo.

Alisema mbali na teknolojia hiyo kurahisisha kazi, lakini inaweka usalama wa afya ya waendesha mitambo kutokana na miundombinu yake kutoruhusu vumbi kumfikia mtumiaji wakati wa zoezi la kupukua mahindi. "Upatikanaji wa huduma hii ya kumrahisishia kazi mkulima anapovuna mazao yake na miongoni mwa njia rahisi za kupata teknolojia hiyo ni kupitia mawasiliano ya simu ya mkononi ambapo muhitaji uzipata katika mfumo maalum," alisema Mndeme.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TAPBDS, Deodati Bernard, alisema waliamua kuleta mradi huo mkoani Njombe kwa sababu ni wadau wanaoshiriki kuendeleza wakulima katika kuhakikisha wanafanya kilimo biashara.

Alisema kupitia mradi wa kipato tija Tanzania ambao pia unasimamiwa na Agra umewakifikia wakulima zaidi ya 30,000 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2017.

"Zoezi la kupata wanufaika wa mashine hizo za mazao lilifanyika kwa kutoa tangazo na wakulima kuomba ruzuku ambapo idadi ya wakulima 57 walijitokeza na waliokidhi vigezo na kupatiwa mashine hizo ni 17 mashine ambazo zimegharimu zaidi ya shilingi milioni 60," alifafanua Benard.

Vilevile, wajasiriamali zaidi ya 250 wakiwamo vijana wanaofanya shughuli zao ndogo 30 waliwezeshwa zaidi ya milioni 60 katika mpango wa ruzuku na kuchangia ongezeko la ajira zaidi ya vijana 350 katika mikoa hii mitatu ya Njombe, Iringa na Ruvuma.

Baadhi ya wanufaika hao wa mashine za kupukuchulia mazao ya nafaka akiwamo Lucy Kitavile na Ibrahim Mhesi walishukuru kupatiwa mashine hizo kwa ushirikiano wa AGRA na TAPBDS na kwamba zitawawezesha kupukuchua kiwango kikubwa cha nafaka tofauti na awali ambapo ilikuwa inawalazimu kutumia nguvu kubwa kupukuchua kiasi kidogo cha nafaka. "Nawashukuru AGRA na TPBDS kwa kuniwezesha kupata mashine za kupukuchua na guta la kubebea mazao kwani awali nilikuwa napiga mahindi kwa kutumia miti," alisema Kitavile.

Mradi huo wa kupukuchua mazao kwa njia ya mashine ulianza Julai mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu ambapo imeshirikisha mikoa ya Iringa, Njombe, Katavi, Ruvuma, Kagera na Mbeya.

## Kyela kuboresha miundombinu

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

WILAYA ya Kyela, imewahakikishia wananchi kuboresha miundombinu ya maji ili wapate huduma hiyo kwa urahisi na kwa gharama nafuu na kusaidia kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya, Claudia Kitta, aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kukagua vyanzo mbalimbali vya maji yanayotumika wilayani humo ambavyo vingi vinapatikana katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Alisema serikali imeipatia Halmashauri ya Kyela pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi mingi na kwamba baadhi ya miradi hiyo imekamilika na mingine ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Kitta alisema ili miradi inayotekelezwa na serikali iwe na faida kwa wananchi na idumu kwa muda mrefu ni lazima kila mwananchi ashiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji ikiwamo kutokata miti kwenye vyanzo hivyo.

"Tuna miradi mingi sana ambayo asilimia kubwa ya vyanzo vyake vipo Busokelo, sasa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunavitunza vyanzo hivi kwa kuvitembelea mara kwa mara ili tuwe na uhakika wa kupata maji muda wote," alisema Kitta.

Alizitaka jumuiya za watumia maji wilayani humo kuhakikisha zinakusanya mapato ya kutosha matengenezo ya baadhi ya vifaa kwenye miradi hiyo yawe yanafanyika mara kwa mara.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji ambayo waliahidiwa kwa madai kuwa kwa sasa huduma hiyo ipo kwa kiwango kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa hawana uhakika wa huduma hiyo.

Joseph Mwakifuna, mkazi wa Mji wa Ipinda, alisema awali walikuwa wanategemea sana maji ya kwenye visima ambayo usalama wake ni mdogo kwa afya zao lakini sasa hivi wanatumia maji safi ya bomba.

Alisema kabla ya maji ya bomba kuanza kutumika, mara nyingi wananchi walikuwa wanaumwa matumbo na mlipuko wa kipindupindu ulikuwa unawasumbua hasa kipindi cha mvua ambapo maji machafu yalikuwa yanaingia kwenye visima. "Sasa hivi maji ya visima tunayatumia kwa ajili ya kufulia nguo na kuoga, hakuna tena kunywa kwa sababu tuna maji safi ya mabomba na tunahamasishwa kila mwenye uwezo avute bomba nyumbani kwake," alisema Mwakifuna.

Alisema hata katika Kituo cha Afya cha Ipinda ambacho ni miongoni mwa vituo bora vya afya katika Mkoa wa Mbeya, maji ilikuwa ni tatizo kubwa awali lakini kwa sasa yapo ya kutosha.

Mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alifanya ziara ya kukagua miradi ya maji katika wilaya hiyo ambapo alizindua mradi wa maji wa Kapapa Group ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.5.

Mradi huo unaanzia katika chanzo kilichopo Busokelo wilayani Rungwe na unahudumia wananchi zaidi ya 13,000 wa vijiji nane kutoka katika kata nne za Ipinda, Mwaya, Talatala na Ikama.

HABARI ZANZIBAR

# Chama cha Walimu chaidai serikali mil. 246/-

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Walimu Zanzibar (ZATU) kimesema kuwa kinadai Sh. milioni 246 kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Unguja ambazo zinatokana na wanachama wa Ushirika wa Walimu (TDS).

Hayo yalielezwa jana na Katibu wa ZATU, Mussa Ramadhan Tafurwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari Kijangwani Mjini Unguja.

Alisema wakati wa kuanzishwa kwa mfumo wa ugatuzi, walimu walikuwa na matumaini makubwa kuwa mambo yangekuwa mazuri na bora kuliko pale kila kitu kilipokuwa kikisimamiwa na Wizara ya Elimu, lakini wanachokishuhudia sasa ni mambo ya kukatisha tamaa.

Alisema baadhi ya wanachama wa chama hicho walijiunga na mfuko wa kuweka na kukopa (Saccos) ambapo walimu waliwataka waajiri wao kuweka kiwango cha fedha walichokubaliana kutoka katika mshahara wao na ziingizwe katika Saccos hiyo, lakini cha kushangaza fedha wanakatwa bila kupelekwa katika mfuko.

Aliwataja wadaiwa sugu wa madeni ya walimu hao ni Baraza la Manispaa ya Mjini Unguja ambalo linadaiwa Sh. 33,440,625, Baraza la Manispaa ya Magharib 'A' Unguja Sh. 68,693,600 na Baraza la Manispaa ya Magharibi 'B' Unguja Sh. 16,883,350.

Zingine ni Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja Sh. 11,519,425, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja Sh. 3,436,750, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja Sh. 24,415,570 na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja Sh. 11,179,540.

Aidha, alizitaka halmashauri hizo pamoja na mabaraza ya mji kulipa malimbikizo hayo ya madeni ya walimu hasa ikizingatiwa kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati alipowaapishi mawaziri aliowateua, alihimiza haki na wajibu ambapo aliwataka mawaziri hao kuhakikisha wafanyakazi wanapewa haki zao.

Katibu huyo alieleza kuwa licha ya walimu kudai fedha zao hizo, lakini wapo baadhi ya walimu hawapelekewi michango yao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na waajiri wao, jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Alieleza changamoto nyingine inayowakabili walimu ni malimbikizo ya posho za nauli pamoja na posho ya likizo, hivyo aliwataka mawaziri wenye dhamana kushughulikia matatizo hayo kama walivyoagizwa na rais baada ya kula kiapo.

Hata hivyo Katibu huyo, alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa uundaji wa Baraza la Mawaziri, lakini wasiwasi wao kuwa hakuna wizara iliyopewa jukumu la kusimamia masuala ya kazi.

"Kazi ni miongoni mwa mambo yasio ya Muungano na Zanzibari inasimama kivyake kwenye Shirika la Kazi Duniani ( ILO), hivyo tunaamini Rais hakuisahau wala kuiacha kabisa, lakini hayo ndio mapendekezo yetu kuwapo kwa wizara inayoshughulikia masuala ya kazi," alisema.



Katibu wa Chama cha Walimu Zanzibar (ZATU), Mussa Ramadhan Tafurwa (kulia), akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kijangwani Mjini Unguja jana kuhusu masuala mbalimbali yanayokihusu chama hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi wanolewa kuhusu mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametakiwa kutunga sheria na kanuni bora zitakazosimamia rasilimali ya mafuta na gesi asilia, ili sekta hiyo kuleta tija, maisha bora na neema kwa wananchi wote.

Hayo yalielezwa jana na Mhadhiri kutoka Chuo cha Diplomasia, Dk. Juma Kanuwa, alipokuwa akitoa mada inayohusiana na uchumi wa mafuta na gesi pamoja na maslahi ya Taifa katika mafunzo elekezi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Dk. Kanuwa alisema ili Zanzibar iweze kusonga mbele kiuchumi na ustawi wa jamii, inahitaji usimamizi mzuri wa sekta ya mafuta na gesi, pamoja na kujenga mazingara bora ya ukusanyaji mzuri wa mapato kutokana na sekta hiyo, ambayo yatakayoweza kuisaidia serikali kuimarisha huduma kwa wananchi wake.

Alieleza kuwa suala hilo linawezekana iwapo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataisimamia vyema sekta hiyo kwa kutunga sheria, kanuni na miongozi bora na hatimaye rasilimali ya mafuta na gesi asilia kuchimbwa kwa maslahi ya taifa.

Hata hivyo alisema ni vyema kwa sheria na kanuni zilizopo kuzingatia athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza hasa kwa viumbe vya baharini na nchi kavu, pamoja na athari za kiulinzi na utamaduni wakati wa uvunaji wa rasilimali hiyo.

Kwa upande wao wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliiomba elimu ya uzalendo na maslahi ya Taifa ifikishwe katika makundi yote kwa jamii ili kila mwananchi kutimiza wajibu wake kwa kuienzi, kuipenda na kuiheshimu nchi yake.

# Mwinyi awakaribisha Bohora kuwekeza Z'bar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakaribisha wawekezaji kutoka Jumuiya ya Madhehebu ya Bohora kuwekeza Zanzibar kutokana na fursa mbali mbali zilizopo nchini.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na wajumbe wa jumuiya hiyo wakiongozwa na kiongozi wao, Sheikh Tayabali Hamza Bhai Patanwalla, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya mwenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam.

Alisema milango ya Zanzibar iko wazi, hivyo anawakaribisha kuja kuwekeza Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba walio wengi katika jumuiya hiyo ni wafanyabiashara.

Alisema kuwa Zanzibar ina fursa nyingi za kuwekeza katika sekta mbalimbali za maendeleo zikiwamo viwanda hivyo, aliwataka kuitumia fursa hiyo na kusisitiza kwamba iwapo itazitumia fursa hiyo vyema, itasaidia katika kutoa ajira kwa vijana.

Alieleza kwamba Serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na madhehebu hayo pamoja na yale mengine nchini katika kuhakikisha kunakuwapo ushirikiano wa kuendeleza na kuimarisha sekta mbalimbali za maendeleo.

Kwa upande wao, viongozi wa jumuiya hiyo walimkabidhi Rais Dk. Hussein Mwinyi salamu za pongezi zilizotolewa na Kiongozi wa Madhehebu ya Bohora duniani, Dk. Syedna Mufaddal Saifuddin, kwa ushindi alioupata na kuwa Rais.

Akisoma salamu hizo kutoka kwa kiongozi huyo, Murtaza Zakirhussein AliBhai ambaye ni Mjumbe wa Jumuiya hiyo alieleza kuwa kiongozi wa Madhehebu ya Bohora duniani, Dk. Syedna Mufaddal Saifuddin, anatoa pongezi kwa Rais Dk. Hussein na kusema kwamba wananchi wa Zanzibar wana matumaini makubwa na uongozi wake.

Salamu hizo zilieleza kwamba kiongozi huyo ana matumaini makubwa kwamba Zanzibar itaendelea kupata mafanikio makubwa katika kuendeleza kujiletea maendeleo yake kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Viongozi hao walisema watahakikisha jumuiya yao inakubali ombi la Dk. Mwinyi kuwekeza katika sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo viwanda na sekta nyenginezo.

**Alieleza kwamba Serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na madhehebu hayo pamoja na yale mengine nchini katika kuhakikisha kunakuwapo ushirikiano wa kuendeleza na kuimarisha sekta mbalimbali za maendeleo.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ni ya ghorofa moja, ina frem tatu za biashara zote zina wapangaji. Bei maelewano, ipo Ukonga Dar es salaam. Piga simu namba **0757 079 057.**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERNEST ANTONY MAYAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 817 CEM.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi**
**MBE/MBE/RB/814729/2020**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**YAH:**
**SHAURI NAMBA 24 LA 2020**
**FLORA NYANANA KAPUNGU................................ MDAI**

**DHIDI YA**
**MBWANA HASSANI MBWANA............................ MDAIWA**
**HASANI ATHUMAN @ BABA KITANDA ..................................MDAIWA**
**KWA: MBWANA HASSANI MBWANA NA HASANI ATHUMAN @ BABA KITANDA -POPOTE MLIPO**

**FLORA NYANANA KAPUNGU,** amefungua shauri mbele ya baraza la Ardhi na Nyumbaa Wilaya ya tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 24/11/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba ( W ) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.
**AMRI** hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 17/111/2020

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**YAH:**
**SHAURI NAMBA 24 LA 2020**
**FLORA NYANANA KAPUNGU................................ MDAI**

**DHIDI YA**
**MBWANA HASSANI MBWANA............................ MDAIWA**
**HASANI ATHUMAN @ BABA KITANDA ..................................MDAIWA**
**KWA: MBWANA HASSANI MBWANA NA HASANI ATHUMAN @ BABA KITANDA -POPOTE MLIPO**

**FLORA NYANANA KAPUNGU,** amefungua shauri mbele ya baraza la Ardhi na Nyumbaa Wilaya ya tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 24/11/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba ( W ) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.
**AMRI** hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 17/111/2020

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA J/PCF.45**
**HATI YA KUUZA MALI KWA KUTIMIZA HUKUMU (MCA/84)**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE wilaya ya DODOMA**
**Shauri la madai No.25/2020.**
**Mdai DORAH MARTIN NYANGE**
**Amdai**
**Mdaiwa AZAPETRO MDEE**
**Kwa: ROYAL RUNNERS GENERAL SUPPLIES S.L.P 1045 DODOMA.**

Hati hii ya KUAMURU kuuza katika Mnada wa Hadhara, baada ya kutangaza kwa muda wa siku 14 kwa kubandika tangazo hilo katika nyumba ya Mahakama hii, ikieleza wakati na mahali patapofanywa mnada huo na mali itakayouzwa, na baada ya kutangazwa TUTAUZA NYUMBA ILIYOPO ILAZO H/NO 13(2) NA VIWANJA 2 NZUGUNI "C" KUGAWA TALAKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 29/11/2020 SAA 10:00 ASUBUHI.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA J/PCF.45**
**HATI YA KUUZA MALI KWA KUTIMIZA HUKUMU (MCA/84)**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE wilaya ya DODOMA**
**Shauri la madai No.6/2019.**
**Mdai MAGRETH PATRICK**
**Amdai**
**Mdaiwa HARIDI RAJABU**
**Kwa: ROYAL RUNNERS GENERAL SUPPLIES S.L.P 1045 DODOMA.**

Hati hii ya KUAMURU kuuza katika Mnada wa Hadhara, baada ya kutangaza kwa muda wa siku 14 kwa kubandika tangazo hilo katika nyumba ya Mahakama hii, ikieleza wakati na mahali patapofanywa mnada huo na mali itakayouzwa, na baada ya kutangazwa TUTAUZA NYUMBA ILIYOPO SWASWA H/NO 104 PLOT NO 379 KUGAWA TALAKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 29/11/2020 SAA 12:00 MCHANA.TAREHE 29/11/2020 SAA 10:00 ASUBUHI.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **SULEMAN HAMAD ABDALLAH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK 11** yenye namba za usajiri **T 881 BSW. Chassis namba GX1106102468.** Engine namba **1G7055456.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa Polisi:**
**TAN/RB/812111/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZABIB ISSA** wa Igomelo Mjini Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.430 BEH** aina ya **Toyota RAV 4.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

**Taarifa ya jeshi la polisi.**
**KAH/RB/406/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**SUSAN ELIAS MPILIMBA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha sita na result slip ya kidato cha sita vyenye **index namba S0255/0530** vilivyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **ST CHRISTINA GIRLS** mwaka 2020,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**DAR/MSI/RB/812994/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICENTH AFREY MKENDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4312.0076** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MRAOKERYO SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**DAR/URA/RB/813473/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**WINFRID FLORIAN NDUNGURU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0124/0030** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **LIKONDE MINOR SEMINARY** mwaka 2017. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**UBS//RB/1854/2020.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAN-GLOBAL VENTURES COMPANY LIMITED**
**Mwanzange Area,Martin's Shamba Street,P.O.Box 612,Tanga**
**Simu: 0715 752205, 0714 560080**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**KESI YA MADAI NO.6/2017**
KWA IDHINI NILIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MFAWIDHI WILAYA YA TANGA. NITAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA YA NDUGU HUSSEIN **NASSOR ALI** ILIYOPO ENEO LA MNYANJANI KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA. NYUMBA HIYO INAUZWA ILI KUTIMILIZA HUKUMU YA MAHAKAMA YA WILAYA YA TANGA.
MNADA UTAFANYIKA TAREHE 02/12/2020 SIKU YA JUMATANO KUANZIA SAA 4.00 ASUBUI NA KUENDELEA KWENYE ENEO ILIYOPO NYUMBA HIYO. ANAYEHITAJI KUNUNUA AWASILIANE NAMI KWA SIMU NA ANWANI TAJWA HAPO JUU.
MASHARTI:
MNUNUZI ATAPASWA KULIPA 25% KWENYE SIKU YA MNADA NA MALIPO YANAYOBAKI YATALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), MUDA HUO UKIPITA BILA MALIPO KUMALIZWA, FEDHA (25%) ZILIZOLIPWA AWALI HAZITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA.

PAUL PROTAS KOMBA
DALALI WA MAHAKAMA-TANGA
TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 24/11/2020

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Joe Biden kuteua Baraza Mawaziri leo

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden atafanya uteuzi wa kwanza wa Baraza la Mawaziri, leo, kulingana na taarifa iliyotolewa na mkuu wake wa utumishi.

Rais Donald Trump, ameendelea na madai yake ya kuwapo na udanganyifu katika uchaguzi wa rais na kuongezeka kwa upinzani ndani ya chama chake mwenyewe huku akikataa kukubali kushindwa.

Biden ameendelea na maandalizi ya kuchukua madaraka ifikapo Januari 20, mwaka huu, licha ya jaribio la Trump la kutaka kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa Novemba 3, mwaka huu.

Trump amepata pigo jingine baada ya kesi yake ya kupinga matokeo kutupiliwa mbali.

Hii ni baada ya timu ya kampeni ya Trump, kuwasilisha kesi mahakamani iliyonuia kupinga matokeo ya kura zilizopigwa kwa njia ya posta katika Jimbo la Pennsylvania. **DW**



Rais mteule wa Marekani, Joe Biden akiwa na Makamu wake, Kamala Harris.

## Jaji kuwasilisha malalamiko uhalifu dhidi ya Zuma

**JOHANESGURG,** Afrika Kusini

JAJI anayeongoza uchunguzi wa ufisadi nchini Afrika Kusini amesema kuwa malalamiko ya ufisadi, yatawasilishwa dhidi ya Rais Jacob Zuma, baada ya kuondoka nje ya kikao cha kamati kilichokuwa kikifanya uchunguzi dhidi yake.

Zuma alijaribu kuhakikisha Naibu Jaji Raymond Zoro, anaondolewa katika uchunguzi huo, akimtuhumu kuwa na upendeleo.

Lakini wakati lengo lake likigonga mwamba, rais huyo wa zamani na wakili wake, hawakurejea tena mbele ya kikao hicho kukabiliana na maswali kuhusu ufisadi.

Takriban mashahidi 34 wamemshutumu kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo Zuma.

Aidha Zuma, alikana kufanya kosa lolote lile.

Kamati, ambayo imekuwa ikisikiliza ushahidi tangu mwaka 2018, imesema kuwa iliwasiliana mara moja na Mahakama ya juu zaidi ya Afrika Kusini, Mahakama ya Katiba, katika juhudi za kumlazimisha Zuma, aitikie wito wa kuhojiwa. **BBC**

# Waziri Mkuu Ethiopia atoa saa 72 Tigray kujisalimisha

**Addis Ababa,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Ably Ahmed, ametangaza saa 72 kwa vikosi vinavyoongoza mapigano Kaskazini mwa eneo lenye utata la Tigray, kujisalimisha kwa serikali.

Hatua hiyo inayojiri wakati majeshi yanayoegemea upande wa serikali ya Ethiopia, yakitangaza kuelekea kudhibiti mji kuu wa Mekelle.

"Njia ya uharibifu wenu inakaribia kufikia mwisho na tunawaomba mjisalimishe ndani ya muda wa saa 72 zijazo.

Huo ulikuwa ujumbe uliotumwa juzi Jumapili na Ably Ahmed kwa viongozi wa Chama cha Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF).

**Mmepewa maagizo ya kujitenga na kundi hilo la waasi, baada ya hapo hakutakuwa na msahama.**

Waziri Mkuu aliwasihi kuweka chini silaha. "Mmefikia kwenye hatua ambayo hamna jinsi ya kujikwamua. Chukua nafasi hii ya mwisho kuweza kujisalimisha," aliongeza.

Saa chache kabla ya tangazo hilo, jeshi la Ethiopia, lilionya kwamba shambulio dhidi ya Mékélé linakaribia kutekelezwa.

Msemaji wa jeshi, alitoa wito kwa wakazi 500,000 ambao wanaishi katika eneo hilo kuondoka haraka.

"Mmepewa maagizo ya kujitenga na kundi hilo la waasi, baada ya hapo hakutakuwa na msahama."

Kwa kujibu tangazo hili kutoka kwa jeshi, Debretsion Gebremichael, mkuu wa vikosi vya TPLF, aliahidi kwamba vikosi vyake vitafanya mashambulizi makubwa.

"Shambulio dhidi ya Mékélé halitabadili chochote kwenye uwanja wa mapigano kwa sababu maadamu wanajeshi bado wapo katika Jimbo la Tigray, mapigano hayatakoma," alisema Gebremichael.

Serikali ilisema, jeshi liliteka miji kadhaa kwenye barabara kuelekea Mékélé.

Wakati huohuo TPLF, ilishutumu vikosi vya jeshi kwa kuua raia wakati wa mashambulizi ya anga katika mji wa Adigrat, madai ambayo yamefutiliwa mbali na serikali. **RFI**



Samaki waliotoka kuvuliwa katika eneo la Santa Rosa de Salinas, nchini Ecuador. Shirika la Chakula na Duniani (FAO), limesema asilimia 95 ya wavuvi wote wapo barani Afrika na Asia katika maadhimisho ya Siku ya Uvuvi Kimataifa, Novemba 21, kila mwaka. **PICHA/UN**

# Idadi watu waliofariki dunia katika maandamano Uganda yafikia 45

**KAMPALA,** Uganda

POLISI nchini Uganda, imesema idadi ya vifo vilivyotokea katika maandamano ya wiki iliyopita imeongezeka na kufikia watu 45.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana msemaji wa polisi, Fred Enanga, alisema waliokufa ni wanaume 39 na wanawake sita.

Chombo kimoja cha habari nchini humo, kimevinukuu vyanzo vya usalama vikisema kuwa ufyatuaji risasi ulifanywa na watu ambao hawakuwa wamevaa sare, walirekodiwa na umma wakinadi bunduki kwenye mitaa.

Waziri wa Usalama nchini humo, Jenerali Elly Tumwiine, aliwaambia waandishi wa habari wiki iliyopita kuwa polisi na vikosi vingine vya usalama wana haki ya kufyatua risasi na kuua.

Polisi ilisema kuwa maofisa wao 11 walishambuliwa na kujeruhiwa na waandamanaji.

Maandamano yaliibuka katika maeneo mbalimbali katika mji mkuu Kampala, huku waandamanaji wakitoa wito wa kuachiliwa mgombea wa urais, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, ambaye alikuwa amekamatwa katika mkutano wa kampeni.

Alishikiliwa siku mbili mahabusu, alishtakiwa kwa kukiuka sheria za kudhibiti virusi vya corona, na kupewa dhamana. Kwa sasa amerejea katika msururu wa kampeni. **BBC**

## Papa aua Australia

**CANBERRA,** Australia

MTU mmoja amefariki dunia baada ya kushambuliwa na papa baharini nchini Australia.

Mtu huyo (55) alipoteza maisha papo hapo baada ya kushambuliwa akiwa katika pwani ya Cable Beach, iliyoko Magharibi mwa Australia.

Baada ya tukio hilo, eneo la pwani lilifungwa kwa muda na wananchi kuzuiwa kuingia baharini kama mojawapo ya hatua ya tahadhari za kiusalama.

Katika nchi ya Australia, kumekuwa na mashambulizi 22 ya papa ndani ya mwaka huu pekee, yaliyosababisha vifo vya watu wanane. **TRT**

HABARI MICHEZO



# MSHAHARA TATIZO MESSI KUTUA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City haitajaribu kumsajili nyota wa Barcelona, Lionel Messi, mtaalamu wa soka la Hispania, Semra Hunter ameiambia Sky Sports News.

Messi mwenye umri wa miaka 33, aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka Barca wakati wa kipindi cha dirisha la majira ya joto lililopita, lakini baadaye akaamua kubaki kwa miamba hao wa LaLiga.

Huku bado hatima yake ikiwa haijulikani, Man City ndio wamekuwa wakihusishwa sana kutaka kumsajili.

Ripoti zinasema kwamba, mshahara wa Messi ndio kikwazo kikubwa ambacho Man City watashindwa kukifikia.

Messi mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

# Flick amtaka Alaba kuamua hatima

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Hansi Flick, amemshauri David Alaba "kuchukua jukumu" katika mazungumzo ya mkataba mpya kama anataka kubaki kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Hali ya Alaba imekuwa mjadala pale Bayern nje ya dimba kwa zaidi ya mwaka sasa, huku mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya yakisimama.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria amekuwa mmoja wa nguzo muhimu kwa klabu hiyo kwa kipindi cha miaka mingi na bilashaka alikuwa na msimu bora zaidi wa 2019-20, wakati mlinzi huyo wa kati akiisaidia Bayern kutwaa taji la Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini mkataba wa sasa wa Alaba unamalizika mwaka 2021 na Bayern haijafanikiwa hadi sasa kumshawishi kuendelea kubakia kwa muda mrefu katika klabu hiyo, huku ikiripotiwa kwamba, amekataa ofa ya mkataba mpya na wakala wake amebainisha kuwa klabu yenyewe ndio inayomyumbisha mchezaji huyo.

Liverpool, Real Madrid na Paris Saint-Germain ni miongoni mwa klabu ambazo amekuwa akihusishwa nazo, lakini Alaba amekuwa na Bayern kwa miaka 11, na Flick anamshauri kuchukua jukumu la kumaliza utata huo.

"David yupo vizuri na ni mchezaji mwenye akili ya soka," alisema Flick akiiambia Welt am Sonntag.

"Ni mchezaji anayejulikana na timu yote inamhitaji kwani amekuwa hapa kwa kipindi cha muda mrefu.

"David anatakiwa kuchukua jukumu na kuamua yeye mwenyewe kipi kitu muhimu kwa upande wake."





# *Conte amwaga lawama wakishinda*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte hakuacha kukilaumu kikosi chake cha Inter Milan licha ya kutoka nyuma na kupata ushindi wa 4-2 dhidi ya Torino na amewashutumu wachezaji kwa kushinda kuendelea na kasi ya msimu uliopita.

Kikosi cha kocha, Marco Giampaolo kilianza kwa kuongoza pale kwenye dimba la San Siro, shukrani kwa mabao ya Simone Zaza na nyota wa zamani wa Inter, Cristian Ansaldi ambao kila mmoja alifunga bao moja na kuifanya Torino kuongoza hadi dakika ya 62.

Romelu Lukaku alimtengenezea bao Alexis Sanchez kabla ya yeye kufunga mawili na moja kwa mkwaju wa penalti na Lautaro Martinez aliyetokea benchi kufunga la nne.

Hata hivyo, Conte alikishutumu kikosi chake licha ya ushindi huo kwa kusema kwamba, hakikuwa na muunganiko wa mzuri.

"Hatukucheza vizuri, sikupenda nilichokiona," alisema.

"Tulitakiwa kuwa makini na kujiamini. Torino walicheza kwa umakini na ustadi mkubwa, sisi hatukuwa kwenye ubora wetu kabisa.

"Naelezea ugumu wa wachezaji baada ya kutoka kwenye mechi za kimataifa, lakini ubora wetu umeshuka, badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma."

## HABARI MICHEZO

# Pique nje ya dimba wiki 5

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa kati wa Barcelona, Gerard Pique, atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki tatu hadi tano kutokana na majeraha aliyoyapata kwenye mchezo dhidi ya Atletico Madrid, Jumamosi.

Pique mwenye umri wa miaka 33, alipata majeraha kwenye kipigo cha goli 1-0 kutoka kwa Madrid katika dimba la Wanda Metropolitano katika mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Pique alishindwa kuendelea na mchezo huo na hivyo kutolewa nje na baadaye taarifa ya klabu ilisema mzaliwa huyo wa Catalunya atakosekana dimbani kwa wiki tatu.

"Pique ameumia na uchunguzi wa timu ya madaktari unaonyesha kwamba, anaweza kuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu hadi tano," ilisema taarifa ya Barcelona ikinukuliwa na gazeti la AS.

Wakati huo huo, Barcelona pia watamkosa pia mlinzi wa pembeni, Sergi Roberto ambaye atakuwa nje kwa miezi miwili.

Kichapo cha Barca cha bao 1-0 kutoka kwa Atletico Madrid mwishoni mwa wiki kinakuwa cha tatu kwenye mechi nane za La Liga ilizocheza msimu huu na wako nafasi ya 10.





# FIRMINO AMKUNA KLOPP LIVER

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amemsifia Roberto Firmino kwa "mchezo bora" baada ya Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Leicester City kwenye Ligi Kuu ya England.

Firmino alifunga bao kwenye ushindi huo pale kwenye dimba la Anfield Jumapili wakati Liverpool ikiendeleza rekodi ya kutopoteza mchezo na kufikisha mechi 64.

Firmino hilo lilikuwa bao lake la pili msimu huu kwenye Ligi Kuu na raia huyo wa Brazil alipiga pasi 48, huku 41 zikifanikiwa na kupiga mashuti sita.

Klopp alimsifia mshambuliaji huyo na kusema alifurahia kuona nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, akifunga bao kwa kuunganisha kona ya James Milner ya dakika ya 86.

"Tulikuwa na furaha na ushindi. Yeye alistahili zaidi. Alicheza mchezo bora kabisa, alicheza mchezo wa kuvutia na ilikuwa muhimu kwa upande wetu," alisema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Unaweza kuona kwenye sura za wachezaji pale anapofunga bao, ni jambo la kuvutia."

Bao la Firmino lilikuja baada ya Jota kufunga la pili kwa Liverpool baada ya Jonny Evans kujifunga dakika ya 21.

# *Gattuso apagawa kiwango Ibrahimovic*

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Napoli, Gennaro Gattuso, anaamini Zlatan Ibrahimovic yupo katika kiwango bora zaidi kwa sasa kuliko alivyokuwa miaka 10 hadi 12 iliyopita baada ya kuonyesha ubora wa kuvutia kwa AC Milan.

Ibrahimovic alifunga mara mbili wakati Milan ikirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakishinda 3-1 dhidi ya wachezaji 10 wa Napoli, Jumapili.

Ibrahimovic amekuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga mabao 10 katika mechi nane za kwanza za Serie A, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 39, ameizima rekodi ya mchezaji wa zamani wa Lazio, Silvio Piola (alipoweka rekodi hiyo wakati akiwa na umri wa miaka 29 msimu wa 1942-43).

Ibrahimovic alifunga dakika ya 20 na 54 na Gattuso ambaye alicheza naye pale Milan kati ya mwaka 2010 na 2012, amemsifia mkongwe huyo.

"Milan wanamwamini Ibra, kwa asilimia 100 kwa kile anachokifanya," alisema Gattuso akiambia Sky Sport Italia.

"Nafikiri yuko imara zaidi kuliko alivyokuwa miaka 10 au 12 iliyopita. Yupo kwenye ubora zaidi kwa sasa, naamini atakuwa na kazi kubwa ya kuisaidia Milan kwa muda mrefu."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ALIA NA KADI NYEKUNDU YA PEPE

## Ni wakati wakishikwa na Leeds, asema haikubali, haikubaliki, katika hatua hii huwezi...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema hakuna utetezi kwa kadi nyekundu ya Nicolas Pepe na kwamba "haikubaliki" na akabainisha kushindwa kwa Arsenal kufunga mabao "ni jambo linaloumiza" baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Leeds United.

**Winga Pepe alionyeshwa kadi nyekundu mapema kipindi cha pili pale kwenye dimba la Elland Road Jumapili baada ya kumpiga kichwa, Ezgjan Alioski.**

Kadi hiyo nyekundu ya Pepe ilikuwa ni ya tano kwa Arsenal kwenye Ligi Kuu ya England tangu Arteta achukue mikoba ya kukinoa kikosi hicho Desemba 2019.

Leeds iligonga mwamba mara tatu na Bernd Leno aliokoa hatari nyingi kwa 'Washikabunduki' hao na hivyo kujikuta wakiondoka na pointi moja na kubakia nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Arteta hakuridhishwa na kitendo cha Pepe, ambapo ugomvi wake na Alioski ukamfanya atolewe nje na mwamuzi, Anthony Taylor.

Aliiambia BBC Sport: "Haikubali. Haikubaliki. Katika hatua hii huwezi kufanya vile."

Arsenal imefunga bao moja tu katika mechi zake tano zilizopita za Ligi Kuu na hilo lilikuwa ni la penalti aliyopiga Pierre-Emerick Aubameyang wakati wakishinda dhidi ya Manchester United.

Miamba hao wa London Kaskazini wamefunga mara tisa kwenye Ligi Kuu msimu huu, ambapo ni idadi ndogo zaidi ya mabao baada ya mechi tisa za Ligi Kuu tangu mwaka 1986.

Arteta, ambaye alimwanzisha nahodha Aubameyang kwenye safu ya kati ya ushambuliaji, anajua kwamba wanahitaji kufunga mabao zaidi kama wanataka kupanda juu katika msimamo.

Wakati alipoulizwa kuhusu kukosekana kwa mabao, kocha huyo raia wa Hispania alijibu: "Ni suala linalotuhusu na kutuumiza. Unahitaji kufunga mabao ili kushinda mechi. Tunahitaji kutengeneza nafasi."

Pepe iligonga mwamba wa goli, lakini Arsenal ilipiga mashuti mawili tu yaliyolenga goli, wakati shuti la Bukayo Saka liliokolewa na Illan Meslier.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL SAFI KWA YAZICI

ARSENAL imepigwa jeki katika harakati zake za kumsajili kiungo wa kati wa Uturuki, Yusuf Yazici baada ya wakala wake kukiri kwamba mchezaji huyo huenda akaondoka katika klabu ya Lille. Mchezaji huyo amefananishwa na kiungo wa kati wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32. ***(Mirror)***

### HENDERSON AWANIWA LEEDS

KIPA wa Manchester United, Dean Henderson, mwenye umri wa miaka 23, atafuatilia uhamisho wake wa mkopo ili kuimarisha nafasi yake ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku klabu za Leeds United na Brighton zikihusishwa naye kwa usajili wa Januari. ***(Sun)***

### CITY WAACHANA NA MESSI

KLABU ya Manchester City imesitisha harakati zake za kutaka kumsajili mshambuliaji nyota wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kwa mujibu wa mtaalamu wa soka wa Hispania, Semra Hunter. ***(Sky Sports)***

### GUENDOUZI AMWANIKA ARTETA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Matteo Guendouzi, mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Hertha Berlin, amedai kwamba amepata motisha aliopoteza chini ya kocha, Mikel Arteta akiwa kule Arsenal. ***(Telefoot, via Star)***

### GIROUD KUAMUA HATIMA YAKE

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Olivier Giroud, mwenye umri wa miaka 34, amekiri kukosa muda wa kushiriki katika mechi nyingi Chelsea kunamtia wasiwasi na kwamba huenda akafanya maamuzi kuhusu hatima yake Januari. ***(Mirror)***

### ERIKSEN KUONDOKA INTER

ALIYEKUWA kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 28, yuko huru kuondoka Inter Milan Januari, Ofisa Mkuu wa klabu hiyo ya Italia, Beppe Marotta, amethibitisha. ***(Goal)***

### AIFUNGUKIA SHEFFIELD

CHRIS Wilder, ambaye klabu yake ya Sheffield United ipo chini ya jedwali la Ligi Kuu England ikiwa na pointi moja pekee, amesisitiza kwamba haogopi kufukuzwa kazi. ***(Sky Sports)***

### AIPELEKA BARCA SOKONI

JERAHA la mguu la beki wa Barcelona, Gerard Pique mwenye umri wa miaka 33, huenda likaifanya klabu hiyo kutafuta mlinzi mwingine dirisha la Januari ili kuziba pengo lake. ***(Manchester Evening News)***

### CAMAVINGA AKUNWA SPURS

KIUNGO wa kati wa Rennes na Ufaransa, Eduardo Camavinga, mwenye umri wa miaka 21, amehusishwa na uhamisho kuelekea Tottenham Hotspur, na amekiri angependelea mchakato wa kujiunga na klabu kubwa ingawa anafurahia kusalia katika klabu yake hiyo. ***(Football London)***

### UNITED YAMWANIA ERIKSEN

KLABU ya Manchester United huenda ikatia nia ya kutaka kumsajili, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, ambaye anaonekana kukwama kule Spurs. ***(Corriere dello Sport, via Star)***

HABARI MICHEZO

## KVZ wawafuata Wasudan na 35

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAWAKILISHI wa Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, KVZ FC, leo wanawafuata wapinzani wa Alamal SC Atbara ya Sudan kwenye mechi itakayopigwa Ijumaa wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa timu hiyo, Hassan Amza "Chura" alisema wanatarajia kuondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Zanzibar wa Abeid Amaan Karume majira ya saa nane mchana.

Alisema timu hiyo inatarajia kusafiri na msafara wa watu 35 wakiwamo wachezaji 21, saba kutoka benchi la ufundi, mwandishi wa habari mmoja, viongozi wa timu hiyo pamoja na mkuu wa msafara kutoka Shirikisho la Soka Zanzibar, ZFF.

Aidha, alisema timu hiyo jana ilifanya mazoezi yake ya mwisho visiwani Zanzibar kujiandaa na mchezo huo wa kimataifa huku wachezaji wakionyesha utayari wa kupambana kupata matokeo yatakayowawezesha kusonga mbele katika michuano hiyo.

Alisema licha ya kuwa na majeruhi wanne kutoka kikosi cha kwanza ambao wataukosa mchezo huo, bado wanauhakika na wachezaji watakaosafiri nao kufanya vizuri katika mechi hiyo kabla ya kurudiana visiwani Zanzibar kati ya Desemba 4-6, mwaka huu.

## Msimu alia umakini KMKM ikiachia usiku

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM imeanza vibaya Ligi Kuu Zanzibar baada ya kubana hadi dakika za mwisho, lakini ikajikuta ikikubali kuachia milango mwishoni na kulala kwa mabao 2-0 kutoka kwa maafande wa Zimamoto kwenye mchezo uliopigwa katika Dimba la Amaan majira ya saa 10:00 alasiri juzi.

KMKM walijikuta wakipoteza mchezo huo dakika za mwishoni wakati Zimamoto wakicheza pungufu baada ya mchezaji wao, Hassan Said, kutolewa kwa kadi nyekundu dakika ya 71.

Mabao ya Zimamoto yalifungwa na Kassim Suleiman dakika ya 88 kabla ya Juma Ali kuhitimisha ushindi huo kwa bao la 'usiku', dakika ya 90.

Akizungumzia mchezo huo Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema kupoteza mchezo wa jana kumetokana na wachezaji kukosa umakini hususan katika dakika za mwishoni.

Alisema KMKM ilikuwa na nafasi kubwa ya kupata ushindi kutokana na wapinzani wao kucheza pungufu, lakini wachezaji walishindwa kutumia nafasi nyingi za wazi walizozipata, hiyo ikitokana na kutokuwa makini pindi wanapofika golini.

Aidha, alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu zao katika mchezo wao wa pili watakapoivaa JKU Ijumaa wiki hii.

# MOROCCO: YANGA IMEPITA, TUNAGEUKIA WASUDAN CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuanza mechi yake ya kwanza kwa sare ya bao 1-1, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema kwa sasa wanasahau matokeo hayo dhidi ya Yanga, na kuelekeza akili na nguvu zao kwenye michuano ya kimataifa, wakati huu wakitarajia kuikaribisha Al-Rabita FC ya Sudan Kusini katika mechi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**Morocco ambaye amerithi mikoba ya Thierry Hitimana aliyetimuliwa wiki iliyopita kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo, Jumamosi ataiongoza Namungo katika mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho itakayopigwa katika Uwanja wa Azam Complex kabla ya timu hizo kurudiana nchini Sudan Kusini kati ya Desemba 4-6, mwaka huu.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema mechi dhidi ya Yanga ilikuwa kipimo tosha kwa maandalizi yao kuelekea mchezo huo huku akifafanua kuwa, licha ya kutopata nafasi ya kuwaona wapinzani wao, ana imani na uzoefu alionao katika michuano ya kimataifa atapambana ili kufanya vizuri kulingana na kikosi alichokuwa nacho.

Alisema kikubwa ambacho anakifanya ni kuangalia wachezaji ambao alionao kwa sasa pamoja na aina ya mazoezi atakayowapa kuelekea mechi hiyo.

"Sina presha juu ya michuano hiyo, licha ya kutopata nafasi ya kuwaona wapinzani wetu, nina uzoefu mkubwa wa michuano ya CAF, kilichobaki kwa sasa ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wangu ili kuachana na matokeo ya Yanga na kuelekeza akili kwenye michuano hiyo," alisema Morocco.

Alisema tatizo la Namungo aliloliona kabla ya kukutana na Yanga, wakati akifuatilia Ligi Kuu Bara lilikuwa ni umaliziaji kwenye safu ya ushambuliaji, hivyo atalifanyia kazi.

"Kuna makosa madogo madogo kwa mabeki ikiwamo kutokuwa makini katika mipira ya faulo pamoja na kona, hilo limetugharimu kwa mechi yetu hii dhidi ya Yanga kwa kuruhusu bao kabla ya kujipanga na hatujasawazisha," alisema Morocco.

Alisema anapenda aina ya makipa ambao wanatoka na kwenda kuongeza mashambulizi hali ambayo amekuwa akiifanya kipa wao, Jonathan Nahimana, baada ya kutoka mita 30 ndani ya eneo lake katika mechi dhidi ya Yanga.

"Huwa napenda aina ya kipa kama huyu, tutambue naye ni mchezaji hiyo katika mpira wa kisasa naye anatakiwa kwenda kufanya mashambulizi na kuwa makini hasa tunapokuwa tukishambulia," alisema.

Kwa matokeo hayo ya jana, Namungo inaendelea kushika nafasi ya tisa kwenye msmamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 15 wakati Yanga ambayo imefikisha alama 25 sawa Azam FC iliyopo kileleni, imeshindwa kuwashusha 'Wanalambalamba' hao kutokana na kuwa na tofauti nzuri zaidi ya mabao ya kufunga na kufungwa.



Kikosi cha Yanga kilicholazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi usiku. Sare hiyo ni ya tatu mfululizo kwa Yanga. **MPIGAPICHA WETU**

# *Kaze atoa siri Metacha kuokoa penalti*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, ndiye sababu kubwa ya kipa wa kikosi hicho, Metacha Mnata, kucheza penalti ya Bigirimana Blaise wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, imefahamika.

Kabla ya penalti hiyo kupigwa, Metacha alipewa maelekezo kuwa Blaise hupiga penalti zake upande wa kulia, hivyo kutakiwa kufuata mpira upande huo atakapopiga, hivyo kufanikiwa kuicheza.

Kipa huyo alionekana kupata maelekezo kutoka kwa Kaze kabla haijapigwa na baada ya hapo akaonekana kuwahamasisha mashabiki wa Yanga kuanza kushangilia na kisha kufanya kile alichoagizwa kukifanya.

Baada ya mechi kumalizika kwenye Uwanja wa Mkapa, Kaze aliwapa kazi waandishi wa habari wakaangalie mechi kati ya Namungo dhidi ya JKT Tanzania watagundua siri ya kwa nini kipa wake aliokoa penalti hiyo.

"Niwape siri? Nendeni mkaangalie mechi ambayo Namungo walicheza na JKT Tanzania, mtajua ni kwa nini nilimpa maelekezo kipa wangu kitu cha kufanya," alisema kwa kifupi.

Ukiiangalia mechi iliyochezwa Novemba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, Blaise alipiga penalti yake upande wa kulia na kumfunga kipa wa JKT Tanzania, akiisawazishia timu yake bao, mechi iliyoisha kwa sare ya bao 2-2.

Kilichotokea Lindi ndicho kilichoonekana kutokea Dar es Salaam juzi, kasoro ilikuwa ni kwamba mechi dhidi ya JKT Tanzania mpira uliingia wavuni.

Jinsi Metacha alivyoonekana kusogea upande wa kulia mara moja kabla hata Blaise hajapiga na kweli mpira ukapigwa upande huo huo, hivyo kutopata ugumu wa kuruka sana, ilionyesha kocha huyo alimwambia kuwa Blaise hupiga penalti zake upande wa kulia.

Ikumbukwe kuwa Kaze na Blaise wote ni raia wa Burundi, hivyo anamjuana vema kisoka.

# Michezo

Jumanne Novemba 24, 2020

Nipashe




Arteta alia na kadi nyekundu ya Pepe UKURASA 22

# Fifa sasa yamfungia Rais CAF miaka 5

●●● Sababu zabainishwa, baadhi ya viongozi wa mashirikisho ya soka Afrika watajwa kuhongwa, pia apigwa faini ya Sh. milioni 507 huku...

**GENEVA,** Uswisi

RAIS wa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Ahmad Ahmad, amefungiwa kujihusisha na masuala yoyote ya soka kwa kipindi cha miaka mitano na FIFA kutokana na matumizi mabaya ya fedha.

**Kifungo hicho kilitangazwa wakati ofisa huyo wa Madagasca akiwa kwenye kampeni zake za kutaka kuchaguliwa tena kwa miaka minne zaidi kushika nafasi hiyo CAF, inayompa pia fursa ya kuwa Makamu wa Rais wa FIFA.**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamati ya Maadili ya FIFA, iligundua "Ahmad alikuwa amekiuka wajibu wake wa uaminifu, kwa kutoa zawadi na mafao mengine, kushindwa kusimamia fedha na alitumia vibaya nafasi yake kama Rais wa CAF."



Ahmad (pichani), ambaye ni ofisa wa zamani wa serikali ya Madagascar, pia kifungo hicho cha FIFA kwake, kimekwenda sambamba na faini ya dola za Marekani 220,000 sawa na Sh. milioni 507.9 za Tanzania.

Muhula wa kwanza wa miaka minne wa Ahmad ulikuwa umegubikwa na tuhuma nyingi za matumizi mabaya ya fedha na utovu wa nidhamu katika Makao Makuu ya Shirikisho la Soka la Afrika huko Cairo, Misri.

"Uchunguzi juu ya mwenendo wa Ahmad katika nafasi yake kama Rais wa CAF katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi 2019, ulihusu masuala yaliyohusiana na utawala, pamoja na kuandaa na kufadhili hija ya kwenda Makka, kuhusika kwake katika shughuli za CAF na kampuni ya vifaa vya michezo na shughuli zingine," FIFA ilieleza katika taarifa yake.

CAF ilionekana kulipa karibu dola za Marekani 100,000 sawa na Sh. milioni 230.8 za Tanzania, kwa watu 18, pamoja na Ahmad na wakuu wa baadhi ya mashirikisho 54 ya kitaifa ya soka barani Afrika, kusafiri kwa hija huko Saudi Arabia.

Ili Ahmad aweze kugombea tena nafasi hiyo katika uchaguzi ujao wa CAF utakaofanyika Machi 12, mwakani jijini Rabat, Morocco, ana nafasi ya kukata rufani katika Mahakama ya Usuluhishi ya Mambo ya Michezo (CAS), pindi tu atakapopokea uamuzi mzima uliofikiwa, mchakato ambao utachukua siku 60.

YALAAAH...



Kiungo wa Arsenal, Dani Ceballos, akichezewa ndivyo sivyo na beki wa Leeds United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Elland Road usiku wa kuamkia jana na kumalizika kwa sare tasa. **HABARI UK. 22**

## Kaze ataka majembe Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU akianika dhamira yake ya kutaka 'majembe' mapya kuelekea dirisha dogo la usajili mwezi ujao, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema bado ana kazi kubwa ya kutafuta njia nyingine ya kuwanoa washambuliaji ili kuweza kupambana na mabeki na hatimaye kucheka na nyavu.

Yanga ambayo kesho itaivaa Azam FC, juzi usiku ilishindwa kuvuna pointi tatu dhidi ya Namungo FC, kwa kulazimishwa sare ya bao 1-1, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaze alisema hawajafurahishwa na matokeo hayo ambayo yamewanyima nafasi ya kuongoza ligi, lakini bado anahitaji muda wa kuwapa mbinu mpya washambuliaji wake ili kumudu kutumia vema nafasi wanazopata kwa kuvuna idadi kubwa ya mabao.

Alisema dakika 45 ya kipindi cha kwanza katika mechi yao dhidi ya Namungo walipata nafasi nyingi za wazi na kupoteza kwa sababu ya washambuliaji wake kutokuwa na purukushani za madhara kwa mabeki wa timu pinzani.

"Kulingana na jinsi safu ya ushambuliaji ilivyo, nahitaji kupata watu, ila sitaweza kuweka wazi kwa sababu nitawavunja moyo wachezaji niliokuwa nao wakati bado tuna michezo sita kabla ya dirisha la usajili kufunguliwa," alisema Kaze.

Alisema mbali na washambuliaji wake alisema ameona mapungufu katika safu ya ulinzi kwa kutokujipanga vizuri na wakicheza bila ya maelewano, hivyo kuiruhusu Namungo kutumia udhaifu wao kusawazisha muda mfupi baada ya kupata bao.

"Tulikosa mwelekeo baada ya kushindwa kujua tunazuia kuelekea wapi, jambo ambalo limetokea kwenye mechi tatu mfululizo tulizopata sare hivi karibuni, ikiwamo dhidi ya Gwambina, Simba na Namungo, hilo nalo nimeliona naenda kulifanyia kazi," alisema kaze.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >